# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*






UTALII

UK.11



## AFYA

**HISTORIA YA GONJWA LA MARBURG, DALILI NA JINSI YA KUJIKINGA NALO**

Uk. 12

MICHEZO

**Kocha Julio amtaka MO Dewji kuwabadilisha watendaji Simba**

⇉ Uk.24

Toleo Na. 00007 | Jumatano Machi 29 - Aprili 4, 2023 |

HABARI NDANI

**Shirika kubwa hatihati kuburuzwa kortini**

Uk. 3

**Jaji Mkuu ataja mwarobaini kumaliza ubambikiwaji kesi**

HABARI UK.4



**Rais Samia alivyoshusha neema Singida**

Uk. 12

# Pinda: Adhabu ya kifo ifutiliwe mbali

- Asema mkosaji hana la kujifunza
- Jaji Werema apigilia msumari




Pinda

Jaji Werema

Ndumbaro

Jaji Chande

Spika Tulia

Uk. 4

# Waislamu nchini wapewa neno

Uk. 3

# SMZ yaahidi neema Bumbwini Kiyongwe

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imeahidi kushughulikia changamoto za wakaazi wa Kijiji cha Bumbwini Kiyongwe za ukosefu wa baadhi ya huduma muhimu za kijamii zinazowakabili ili kuleta ustawi bora wa maendeleo yao.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, alitoa ahadi hiyo akiwa Bumbwini Kiyongwe Kaskazni `B' Unguja akiwa katika mfululizo wa ziara za kuwakagua na kuwafariji wangonjwa na wananchi waliopatwa na misiba katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema serikali imepokea kutoka kwa wananchi na kuona kuwepo kwa kero kubwa ya ukosefu wa usafari wa barabara, jambo linalochangia kudhoofisha shughuli za kimaendeleo katika kijiji hicho.

Othman alisema kero kubwa ya barabara iliyopo inayochangia wahudumu wa afya na walimu kutofika na kurudi kwa wakati katika vituo vyao vya kazi, serikali italishughulikia na kulipatia ufumbuzi.

Katika hatua nyingine, Othman aliwaeleza viongozi wa ACT-Wazalendo katika ngazi ya wilaya na mikoa kuiga mfano wa wenzao wa mjini kuanzisha mifuko ya faraja itakayotumika kusaidia kutatua changamoto mbalimbali walizonazo wananchi kwenye maeneo yao.

Aidha, aliwataka viongozi hao kuendeleza ziara katika majimbo yao ili kuonana na kupokea changamoto mbalimbali zilizomo kwenye maeneo tofauti na kwamba kufanya hivyo ndiyo wajibu muhimu wa kiongozi kuwatumikia wananchi.

Mapema, wakazi wa Kijiji cha Kiyongwe walimueleza Makamu wa Kwanza kwamba kijiji hicho hakina barabara kwa muda mrefu sasa, jambo linalochangia wananchi kupata shida ya kuingia na kutoka katika kutekeleza shughuli zao za kimaendeleo.

Othman katika ziara hiyo, alitembelea Majimbo ya Bumbwini, Donge, Tumbatu, Nungwi, Mkwajuni, Kiwengwa, Kijini, Chaani na Mahonda kuwajulia hali wagonjwa na kuwapa pole waliofikwa na msiba ikiwa ni mfululizo wa kuendeleza ziara zilizokuwa zikifanywa na mtangulizi wake, hayati Maalim Seif Shariff Hamad.



Watalii wakipanda Mlima Kilimanjaro.

# Miti 100,000 kupandwa Mlima Kilimanjaro kila mwaka

**Na Mwandishi Wetu, Moshi**

WADAU wa Utalii na Uhifadhi, wamekubaliana kuanzisha kampeni kabambe ya kupanda miti 100,000 kila mwaka katika Mlima Kilimanjaro, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kurudisha uoto wa asili katika mlima huo mrefu zaidi barani Afrika.

Kampeni hiyo iliyoanza kutekelezwa katika msimu huu wa mvua, pia ina lengo la kuhakikisha kuwa theluji iliyo katika kilele cha mlima huo, haitasombwa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyoathiri mazingira.

Tafiti mbalimbali zilizofanywa katika mlima huo, zinaonyesha kuwa theluji iliyoko kileleni mwa mlima huo inapungua kila mwaka na huenda ikaisha kabisa ifikapo mwaka 2050 iwapo hatua za makusudi hazitachukuliwa kupunguza au kumaliza kabisa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya miteremko ya mlima.

Akitangaza kampeni hiyo katika maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA) hivi karibuni, Kamishna wa Uhifadhi katika Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), William Mwakilema, alisema itahusisha wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya chini.

Alisema kwa kuanzia, miti imepandwa katika Shule ya Msingi ya Samanga,Moshi Vijijini na katika Shule ya Msingi Utegi, wilayani Rombo, ikiwa ni sehemu ya kampeni hiyo iliyoshirikisha wadau zaidi ya 700 wa utalii na uhifadhi.

"Kwa kupanda miti mingi katika maeneo yanayozunguka mlima, tunaamini kuwa tutarejesha unyevu unaohitajika kurejesha na kutunza theluji katika kilele cha mlima wetu, na kwa kushirikiana na wadau wetu tuna uhakika wa kufikia malengo.

"Misitu inayozunguka mlima, ikiwa katika urefu wa kuanzia mita 1,700 hadi 2,700 kutoka usawa wa bahari, ina wanyamapori wengi na ikistawi vizuri itachangia sana katika jitihada za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi na kurejesha uoto wa asili wa mlima ambao ni muhimu kwa theluji," alisisitiza Mwakilema.

Akizungumza katika uzinduzi wa kampeni hiyo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, aliwapongeza wadau kwa kuweka malengo ya kupanda miti 100,000 kila mwaka katika miteremko ya mlima huo na kwamba ni hatua muhimu na sahihi.

Alisema malengo hayo yanaenda sambamba na sera ya taifa ya kupanda miti milioni tano ifikapo mwaka 2030, ikiwa ni mpango wa taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo athari zake zinaonekana waziwazi katika maeneo mengi nchini.

> **Kwa kupanda miti mingi katika maeneo yanayozunguka mlima, tunaamini kuwa tutarejesha unyevu unaohitajika kurejesha na kutunza theluji katika kilele cha mlima wetu...**

Aliwaonya baadhi ya wafugaji wanaoshiriki kuharibu mazingira kwa kuingiza mifugo yao katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria, ikiwamo hifadhi za taifa, wakishirikiana na baadhi ya watendaji wa taasisi za uhifadhi.

"Tunajua kuna baadhi ya wafugaji wanawashawishi watendaji wetu katika taasisi za uhifadhi ili waingize mifugo yao katika maeneo yasiyoruhusiwa hasa nyakati za kiangazi na tunawaonya waache mara moja," alisisitiza.

Waziri huyo alisema serikali haitasita kuchukua hatua kali dhidi ya watu wenye mifugo na watumishi wachache wasio na maadili, ili kukomesha vitendo vinavyoathiri ustawi wa mazingira ya milima huo.

Waziri huyo mpya wa Maliasili na Utalii pia aliwataka wapanda mlima huo kuhakikisha wanatunza mazingira ya mlima huo kwa kuacha kutupa takataka ovyo na kuitaka TANAPA kuweka miundombinu ya kukusanya takataka hizo ili kuhakikisha kuwa mazingira yanabaki safi na salama.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya TANAPA, Jenerali Mstaafu George Waitara, alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Samia Suluhu Hassan, kwa kumteua tena kuongoza bodi hiyo kwa miaka mitatu ijayo.

"Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuniamini, napenda kumwahidi kwamba, Kwa kushirikiana na wenzangu, tutahakikisha malengo mapana ya shirika yanafikiwa kwa manufaa ya uhifadhi na utalii na nchi yetu kwa ujumla," alisisitiza Jenerali Mstaafu Waitara ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi.

Maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), yaliambatana na shughuli za kusafisha njia za kupanda na kushuka kutoka mlimani na midahalo ya kutunza Mlima huo iliyohudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi.

Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilmanjaro ni ya pili kwa kuingiza mapato mengi ya kigeni baada ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi hiyo imeongezeka kutoka watalii 12,050 mwaka 2021 na kufikia watalii 47,000 hadi Februari, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Jenerali Mstaafu Waitara, ongezeko hilo limechangiwa na filamu maarufu ya Royal Tour iliyotengenezwa chini ya muongoza utalii namba moja nchini, Rais Samia Suluhu Hassan, ambayo imetumika kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

# Mashirika 7 Ruangwa yatishia `kuiburuza' Tacosode kortini

**Na Mwandishi Wetu, RUANGWA**

MASHIRIKA saba yasiyo ya kiserikali wilayani Ruangwa, yametishia kulishtaki kortini Baraza la Taifa la Maendeleo ya Mashirika ya Kiraia (Tacosode), iwapo hayatalipwa zaidi ya Sh. milioni 24 inazodaiwa.

Hatua ya mashirika hayo inatokana na Tacosode mwaka jana, kukiri kudaiwa Sh. milioni 32, lakini lilipa Sh. milioni nane kati ya fedha hizo na kutomalizia kiasi kingine kilichosalia.

Tacosode inadaiwa kiasi hicho cha fedha ambacho ilipaswa kuyalipa mashirika saba baada ya kuingia nayo mkataba wa kutekeleza mradi wa Kuhamasisha Jamii Kujiunganisha na Nishati ya Umeme Vijijini (REA) katika vijiji 30 mwaka 2019.

> **Ongezeko hili la bajeti sawa na asilimia 33. 09 limesaidia sana kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi katika Mkoa wetu wa Singida....**

Kabla ya Tacosode kuvunja mkataba na mashirika hayo ndani ya kipindi cha utekelezaji wa mradi huo, tayari malengo yaliyokuwa wamewekwa ya kupata wateja wapya 1,270 yalikuwa yamefikiwa.

Mashirika yaliyotoa tishio la kuifikisha kortini Tacosode ni Ruangwa Organization for People's Appeasement (ROPA), Asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (Akuvikiru) na Kikundi cha Wabangua Korosho Ruangwa (Wakoru).

Mengine ni Ruangwa Development Fund (Rudefu), Shirika la Msaada wa Kisheria Ruangwa (Rupao), Shirika la Haki za Binadamu Nandagala (Shihabina) na Muungano wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Wilaya ya Ruangwa (Mmakiru).

Akizungumza na gazeti la Uelekeo, Mkurugenzi wa Mmakiru, Erasmo Tasilo, alisema hatua ya kuishtaki Tacosode mahakamani, ni ya mwisho baada ya jitihada kadhaa ikiwemo kuishtaki Takukuru kugonga mwamba.

"Awali, shauri hili tuliliwasilisha ofisi za Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Ruangwa na baada ya miaka mitatu ya vuta nikuvute, Tacosode ilikubali kulipa Sh. milioni nane, lakini baada ya hapo, hawajalipa tena," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Ropa, Thabiti Munga, alisema kwa kipindi chote cha miaka mitatu, jitihada zimefanywa kuipa nafasi Tacosode ya kulipa deni, lakini haikufanya hivyo.

Afisa wa Takukuru, Victor Kaiza, alithibitisha mashirika hayo saba kuwasilisha malalamiko yao dhidi ya Tacosode na kwamba jitihada kadhaa zimechukuliwa na Sh.milioni nane kati ya Sh. milioni 32 zinazodaiwa na mashirika hayo saba, tayari zimelipwa na Tacosode.

Mkurugenzi wa Tacosode, Theofrida Kapinga, alithibitisha shirika lake kudaiwa na mashirika hayo na kuahidi kulipa deni hilo, lakini bila kufafanua lini.

Hata hivyo, Kapinga alionyesha kusikitishwa kwa jinsi mradi ulivyovurugika na kusababisha mashirika saba washirika kutolipwa fedha zao kwa wakati.

Awali, pamoja na kukiri kudaiwa, Mratibu wa mradi huo, John Ndunguru, alisema alilazimika kuvunja mkataba huo baada ya kubaini kuna baadhi ya mashirika hayakuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo.

Kadhalika, alisema kuna baadhi ya mashirika (bila kuyataja), yalibadili matumizi ya fedha walizopewa kwa kununua samani za ofisi badala ya kufanyia mikutano ya hadhara ya kuhamasisha jamii kujiunganisha na umeme vijijini.

# Sheikh wa Mkoa atoa neno kwa Waislamu

**Na Claudia Kayombo, Singida**



Sheikh wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, akizungumza katika moja ya matukio ya Dini ya Kiislamu, mkoani Singida hivi karibuni. (Picha: Mpigapicha Wetu)

SHEIKH wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, amewataka Waislamu nchini, kuzingatia maadili ya funga ili kupata thawabu kwa Mungu.

Amesema maadili hayo ni pamoja na kufunga, kufanya matendo mema kwa kuwasaidia wajane na yatima huku wakiishi kwa upendo na kusaidiana.

Sheikh Nassoro alitoa rai hiyo wakati wa mahojiano maalum na gazeti hili ofisini kwake mjini hapa jana.

"Kama alivyotuasa Kiongozi wetu Mtume Muhammad, lengo la kufunga ni kujizuia na kila dhuluma, hivyo natoa wito kwa Waislamu wenzangu warudi katika lengo la Ramadhan," alisema Sheikh Nassoro.

Alifafanua kuwa Ramadhan ni shule, hivyo Waislamu waitumie vizuri na kuwaasa wenye uwezo kuacha kuandaa aina nyingi ya futari na mwisho wa siku kuimwaga.

"Wazee wetu walifuturu mabarazani, lakini leo tunafanya hivyo chumbani, nyumba moja wanaishi familia tano za Kiislamu, lakini kila mmoja anafuturu chumbani, tutoe nje kilicho kidogo tule pamoja ndiyo Uislamu unavyosema, umoja ni nguvu," alisema.

Aidha, aliongeza kuwa kila Muislamu aliyefanikiwa kuingia katika funga ya mwaka 1444, anapaswakumshukuru Mungu kwa kuwa wapo waliofunga mwaka 1443 wameshatwaliwa na Mungu.

"Hii ni nafasi ya dhahabu kwa sisi tuliobaki kuwa hai, wapo wenzetu waliofunga Ramadhan mwaka jana kwa mazoea ya kufunga, tufunge kwa kuzingatia funga ili tunufaike na Ramadhan yetu," alisema na kuongeza:

"Tuzingatie lengo la Mungu kutuletea Ramadhan, tusishinde na njaa kwani hata watoto wanaweza kushinda njaa, tuache dhuluma, tuwapende na kuwasaidia wenzetu.

Alisema: "Lengo la kufunga ni pamoja na kujizuia na kila dhuluma, lakini inasikitisha baadhi ya wafanyabiashara wanatumia Ramadhan kujinufaisha."

"Mfano muhogo uliokuwa unauzwa Sh. 1,000, sasa unauzwa Sh. 2,000, haitasaidia, fanya biashara zingatia kuwa usipate hasara wala kutaka faida kubwa," alisisitiza Sheikh Nassoro.

Kuhusu suala la jamii kuwakumbuka wahitaji wakati wa matukio ya sikukuu na Ramadhan, Sheikh Nassoro alisema ipo haja viongozi wa dini kushirikiana na wa serikali za vijiji na mitaa, kuwabaini wenye mahitaji maalum waliopo ili wenye mapenzi mema wajue maeneo walipo, wawasaidie wakati wowote katika mwaka.

Aidha, alitoa wito kwa Waislamu nchini, kumsikiliza na kuzingatia usia anaotoa kiongozi wao Mufti Mkuu wa Tanzania.

# Pinda: Adhabu ya kifo ifutiliwe mbali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amependekeza marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 Kifungu cha 197, ili adhabu ya kifo ifutwe.

Badala yake, Pinda amependekeza mshtakiwa anayekutwa na hatia ya mauaji au uhaini, afungwe maisha gerezani.

Aidha, ameshauri mfumo wa hakijinai uweke utaratibu wa kulelewa kwa mtoto anayezaliwa na mfungwa anayetumikia kifungo gerezani.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa maoni yake mbele ya Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Haki Jinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Othman Mohamed Chande.

"Adhabu ya kunyonga mtu, inanipa taabu kwa sababu ni kweli alitoa roho ya mtu…na yeye tumnyonge? Kosa juu ya kosa. Sidhani kama inatibu (adhabu ya kunyonga), ugonjwa huo," alisema.

Pinda alisema adhabu ya kunyongwa hadi kufa, haina tija kwa sababu mkosaji hapati nafasi ya kujirekebisha, akieleza kwamba kifungo cha maisha kitatoa nafasi ya mfungwa kujifunza na kujutia makosa yake.

"Kubwa kwangu ni ile principle (kanuni) tu, kwamba unaua na wewe unauawa. Nimewaambia waliangalie tuone, nchi nyingi zilishaondoa vitu hivyo," alisema.

Kuhusu mtoto anayezaliwa gerezani, Pinda alisema: "Mama anapokumbwa na janga la mauaji na huku ni mjamzito, anapelekwa rumande, anajifungulia huko, shida yangu ikawa ni kwamba mtoto huyu tusimwache katika eneo hili la magereza."

Pinda alisema mazingira yatamwathiri mtoto huyo kisaikolojia na kupendekeza kuwa waunganishwe na vituo vinavyolea watoto.

> **Kubwa kwangu ni ile principle (kanuni) tu, kwamba unaua na wewe unauawa. Nimewaambia waliangalie tuone, nchi nyingi zilishaondoa vitu hivyo...**

Alisema: "Na hili nimelisema kwa sababu mazingira ya magereza ni magereza tu."

Alisema wanawake wanaojifungua wakiwa magereza, hawapati mazingira mahsusi ya kuwawezesha kulea watoto ikiwamo vyakula vinavyoweza kuongeza maziwa. Aidha, aliishauri Tume kukusanya maoni kutoka kwa makundi yote wakiwamo madereva wa bodaboda, daladala, malori na mabasi; pamoja na makundi yenye malalamiko kwa Polisi, Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Zimamoto na Ofisi ya Mwendesha Mashitaka (DPP), ili iweze kutoa ushauri utakaoleta tija kwa nchi.

Alipendekeza kuwa mnyororo wa hakijinai, unapaswa kuangaliwa kuanzia Polisi, Takukuru, DPP, Mahakama na Magereza, ili wananchi wasiumizwe katika hatua yoyote ya kutafuta haki.

Alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuunda Tume hiyo akieleza kuwa kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi kuhusu mifumo ya hakijinai.

"Malalamiko ni mengi, kila unapozunguka unakutana na watu wanalalamika. Pamoja na kukutana na makundi ambayo wamekwishayaainisha, lakini wajaribu kuangalia kila chombo eneo la malalamiko halafu tuone kama tunaweza kukutana na wadau kwenye hilo eneo," alisema.

Alitoa mfano wa malalamiko ya rushwa kwa askari wa barabarani pamoja na wapelelezi, Tume iwaite madereva wa vyombo vya moto ili wajue tatizo lilipo.

Kuhusu magereza, alisema eneo la kurekebisha tabia kwa wafungwa, lipewe uzito ili wanapokuwa gerezani watoke na ujuzi.

Alisema shirika la uzalishajimali la Magereza, lizalishe bidhaa zake kwa kutumia wafungwa na uwepo mfumo wa kuwafuatilia wanaotoka gerezani wakiwa na ujuzi ili kupima mafanikio ya marekebisho ya tabia ya mhusika.

**JAJI WEREMA**

Kwa upande wake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali mstaafu, Jaji Frederick Werema, akizungumzia adhabu ya kunyonga, alisema siyo adhabu stahiki kwa kuwa haipi mfungwa nafasi ya kujifunza.

Alisema asilimia kubwa ya wanaofanya mauaji, ni watu wenye kipato cha chini akitolea mfano wa mauaji yanayotokana na wivu wa mapenzi na ugomvi kwenye vilabu vya pombe za kienyeji.

"Adhabu inafundisha, sasa ukinyongwa umefundishwa nini? Adhabu ya kunyonga ibaki kwenye sheria kama tishio kwa sababu inaweza kutokea ikabidi unyonge maana kuna watu wanafanya mauaji ya kishenzi," alisema. Aidha, Jaji Werema amewashauri majaji na mahakimu, kumaliza msongamano wa kesi mahakamani kwa kufuta kesi zisizo na ushahidi wa kutosha.

Alisema mwaka 1996, aliwahi kuachia watuhumiwa 50 wa makosa ya jinai kwa siku moja, baada ya kupitia mafaili ya kesi zao na kubaini kwamba hakukuwa na ushahidi unaoweza kuwatia hatiani.

Kuhusu dhamana, alipendekeza marekebisho yafanyike ili Mahakama iwe na mamlaka ya kutoa au kunyima dhamana badala ya inavyofanyika sasa kwa DPP kuwa na nguvu ya kuzuia haki hiyo.

Kadhalika, alipendekeza Sheria ya Utakatishaji Fedha, irekebishwe ili kupunguza makosa kutoka 28 yaliyopo sasa hadi manne, kwa kuwa ilivyo sasa inatumiwa vibaya na baadhi ya maofisa wa DPP 'kuwapa' watu kesi zisizo na dhamana.

Kuhusu Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Jaji Werema alisema amewasilisha marekebisho mengi, lakini hakuyataja.

Hata hivyo, alipendekeza kuwa Mahakama itoe kipaumbele katika kusikiliza kesi za jinai kama inavyofanya kwenye kesi za madai.

**WAKILI MAGAI ALIA NA DPP**

Naye Wakili Mwandamizi Sadock Magai, amependekeza DPP apunguziwe madaraka hasa yanayomruhusu kuzuia dhamana.

Alitaka marekebisho kwenye kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), ili kazi hiyo iachiwe Mahakama.

Wakili Magai kutoka Kampuni ya Uwakili ya IMMMA, alisema kifungu hicho kimekuwa 'kichaka' cha baadhi ya maofisa wa DPP wasio waadilifu, kunyima watuhumiwa dhamana.

"Imekuwa ni kama mchezo, mtu anapelekwa mahakamani, anasomewa mashitaka, ananyimwa dhamana, akiambiwa kwamba kosa husika halina dhamana anapelekwa rumande… miaka mitano nyuma kuna watu wameumia sana, waliwekwa ndani bila kisikilizwa, wamepigwa faini, familia zao zimesambaratika, wengine wamekufa kwa sababu ya makosa ambayo Mahakama ingeamua kama wana makosa ama hawana," alisema.

Alisema DPP alitumia mwanya huo kushtaki wafanyabiashara na kuwanyima dhamana kinyume cha taratibu za Sheria ya Kodi inayoruhusu mazungumzo kati ya mlipakodi na Kamishna wa Kodi.

Alisema baada ya kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kwa kosa la kushindwa kulipa kodi, wafanyabiashara hao waliitwa na DPP kutaka plea-bargaining, kinyume cha taratibu.

# Zoezi ufutaji NGOs endelevu

**Na Abdul Mitumba, Lindi**

SERIKALI mkoani Lindi, imewataka viongozi wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kote nchini, kufanya kila linalowezekana kutimiza matakwa ya kisheria. Moja ya matakwa hayo ni kuandaa na kutuma taarifa za utendaji kazi za kila mwaka ili kuepuka `kimbunga' kinachoendelea cha kufuta mashirika. Aidha, serikali imewakumbusha viongozi hao kuwa takwa la kisheria siyo kulipa ada ya kila mwaka serikalini tu, bali kuandaa na kutuma taarifa za fedha na ulipaji kodi mbalimbali kwa wakati, pia ni mambo muhimu ya kuzingatiwa.

Tahadhari hiyo ilitolewa ikiwa ni wiki chache tu zimepita tangu serikali ilipoyafutia usajili mashirika 4,879 kwa kukosa sifa, huku 19 kati ya hayo yakiomba yenyewe. Kauli hiyo ilitolewa hivi karibu na Afisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Lindi, Metusha Magayane, katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa wanachama wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya Mkoa wa Lindi (Lango).

Alikuwa akichangia hoja ya wajumbe wakati wa mjadala wa nini kifanyike ili kuokoa mashirika mawili wanachama yaliyofutwa na serikali hivi karibuni kwa makosa mbalimbali.

"Sheria ya Bunge ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002 na iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005, inayataka mashirika yote kutimiza masharti yaliyomo katika usajili ikiwemo kuandaa na kutuma taarifa za utekelezaji wa kazi zao kila baada ya miezi mitatu au kila mwaka," alifafanua sema Magayane na kuongeza;

"Kinyume chake, ni lazima serikali italifuta shirika lisilofanya hivyo, maana haitakuwa ikijua linafanya nini kwa maslahi ya wana jamii. Mapema, akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Lango, Pili Kuliwa, aliwataka viongozi wenzake wa mashirika wanachama, kuweka bidii katika kutimiza masharti ya serikali katika uendeshaji pamoja na kuimarisha safu zao za uongozi.

Pili aliyataka mashirika wanachama wa Lango kuwa ni mitandao ya mashirika kutoka Wilaya za Nachingwea, Liwale na Kilwa.

Wakati mitandao iliyofutiwa usajili kwa sasa ni kutoka Wilaya za Lindi Mjini na Ruangwa.

Awali, akizungumza kwenye mkutano, Mkurugenzi wa Lango, Michael Mwanga, ameyataka mashirika wanachama, kuacha ubinafsi hasa kukalia taarifa za kuwepo kwa matangazo ya kuomba ruzuku.

## Jaji Mkuu ataja mwarobaini kumaliza ubambikiwaji kesi

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI Mkuu, Profesa Ibrahim Juma, amependekeza watuhumiwa wa makosa ya jinai wakiwamo wa mauaji, wachukuliwe maelezo mbele ya kamera ili kuondoa malalamiko ya kubambikiwa kesi kwa baadhi ya watu.

Aliyaeleza hayo jijini Dar es Salaam jana baada ya kutoa maoni mbele ya Tume ya Kurekebisha Mfumo wa Hakijinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu, Othman Chande.

Alisema ipo sheria inayoruhusu mahojiano ya ungamo yanapochukuliwa yarekodiwe, lakini vyombo vya haki jinai havijaanza kuitekeleza.

"Sheria za wanaotuhumiwa na kesi mbalimbali za jinai badala ya maelezo yao kuandikwa kwa mkono na polisi, sheria imefanyiwa mabadiliko kwamba yaweze kuchukuliwa kwa njia ya video. Na ile inapunguza malalamiko kwamba nimebambikiziwa kesi," alisema. Jaji Profesa Juma alisema changamoto iliyopo katika kutekeleza sharti hilo la sheria, ni ukosefu wa vitendea kazi kwenye Jeshi la Polisi. "Sheria ile imekuwepo baada ya marekebisho mwaka 2018, lakini matayarisho ya kuwa na vile vifaa vya kuchukua maelezo kwa video hayafanyiki. Sisi tunasema kwamba sheria nzuri zinapotungwa matayarisho ya utekelezaji wake na rasilimali zitoshe ili zifanye kazi," alisema.

Alizungumzia pia sheria ya kumlinda shahidi ambaye hataki kujulikana, akieleza kuwa sheria inataka shahidi huyo aandaliwe mazingira ya faragha ili aweze kutoa ushahidi mbele ya Mahakama, jambo ambalo bado halijatekelezwa.

Alisema nchi nyingi zenye sheria zinazofanana na za Tanzania ikiwamo India, wamefanya maboresho makubwa ikiwamo mtuhumiwa aliyekaa mahabusu kwa muda mrefu, anapotiwa hatiani muda huo, unajumulishwa kwenye adhabu atakayopewa na mahakama.

# Wataka mazingira kufundishia mahitaji maalum yaboreshwe

**Na Claudia Kayombo, Singida**

SERIKALI imeombwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa watoto wenye mahitaji maalum katika shule zake za awali na msingi nchini.

Kadhalika, imetakiwa kuweka miundombinu wezeshi kwa kundi hilo ili kutekelezeka kwa vitendo Sera ya Elimu Jumuishi.

Wakizungumza mkoani hapa, wadau wa elimu na wazazi, wamesema licha ya sera hiyo kuwa mkombozi hasa kwa watoto wasio na uwezo ambao awali walikuwa wakifichwa majumbani kwa kushindwa kuwapeleka shule maalum, changamoto ya mazingira yasiyo rafiki kwenye shule Jumuishi, bado ni kikwazo kikubwa.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali linaloshughulikia Maendeleo ya Elimu Mtinko (Medo), Iddi Hashim. alisema kabla ya Sera ya Elimu Jumuishi, wazazi na walezi wa watoto wenye ulemavu na mahitaji maalum, walikuwa wakilazimika kutafuta shule maalum ambazo hata hivyo, ni chache.

"Sera hii imesaidia hasa kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka minane maana shule Jumuishi zipo jirani ambapo mzazi au mlezi, anaweza kumpeleka mtoto wake wa darasa la awali, la kwanza au la pili, shule asubuhi kisha jioni anamfuata," alisema Hashim.

Aliongeza kuwa changamoto kubwa kwa serikali ni kuongeza bajeti kwa shule hizo ili ziweze kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuweka miundombinu wezeshi kwa watoto wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum kusoma bila kikwazo.

Alifafanua kuwa ingawa serikali hivi sasa imekuwa ikihakikisha shule mpya za msingi zinakuwa na ngazi mtelezo na vyoo kwa wenye mahitaji maalum, majengo ya zamani bado ni kikwazo, uhaba wa walimu wa elimu maalum na zana za kujifunzia na kufundishia kama vile maandishi ya nukta nundu, lugha ya alama na miwani kwa wenye uoni hafifu.

Alisema chini ya Sera ya Elimu Jumuishi ya mwaka 2014, watoto wenye ulemavu, wenye mahitaji maalum na walio kwenye mazingira magumu, wanatakiwa kusoma na wenzao wa kawaida kwenye shule moja bila kubaguliwa ili kila mtoto wa Kitanzania apate haki ya elimu bila kikwazo.

Mmoja wa wazazi ambaye ni Ofisa Maendeleo ya Jamii mstaafu, Patrick Mdachi, alisema ingawa Sera ya Elimu Jumuishi imesaidia hasa kwa watoto wadogo wasioweza kutembea umbali mrefu kufuata shule za vitengo maalum, lakini bado kuna umuhimu kwa serikali kuongeza bajeti ili itekeleze kwa vitendo sera hiyo na kuleta manufaa yaliyokusudiwa.

"Programu Jumuishi ya Taifa kuhusu Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM), iliyoanza Januari, 2021, inaangalia zaidi suala la elimu, afya, lishe, ulinzi na usalama wa mtoto, hivyo ni vizuri na hii Sera ikawekewa mazingira mazuri ili itekelezeke vema," alisema.

Mzazi mwingine, Daud Lameck, mkazi wa Mtipa, alisema serikali ikiboresha shule zinazotekeleza sera hiyo, itavutia watoto hao kusoma kwa bidii.

Takwimu za Halmashauri ya Manispaa ya Singida zinaonesha watoto 84 wenye mahitaji maalum, wamesajiliwa kwenye shule na vitengo mbalimbali kuanza masomo ya awali na msingi mwaka huu 2023 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 30 ikilinganishwa na mwaka jana.

Ofisa Elimu Msingi wa manispaa hiyo, Omary Maje, alisema licha ya sababu nyingine, mafanikio ya uandikishaji watoto wenye mahitaji maalum yametokana na utekelezaji mzuri wa Programu Jumuishi ya Taifa kuhusu malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ya mwaka 2021. Maje alisema chini ya programu hiyo, pamoja na mambo mengine ya usalama, ulinzi, makuzi, afya, lishe na masuala mengine mengi mtambuka, viongozi na watendaji wa mitaa wamekuwa wakizunguka kwenye maeneo yao kuwabaini watoto hao na kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kupewa elimu.

# Naibu Waziri Pinda aitaka NHC iwe ya kimataifa zaidi



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Mizengo Pinda, akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), hawapo pichani) jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah na anayefuata ni Meneja Habari na Uhusiano wa Shirika, Muungano Saguya. (Picha: Kwa hisani ya NHC).

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Mizengo Pinda, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), liwe la kimataifa zaidi kwa kuchangamkia fursa ya ujenzi wa majengo ya Balozi nje ya nchi.

Pinda amesema serikali inamiliki mapande makubwa ya ardhi huko nje ambayo bado hayajafanyiwa kazi ipasavyo.

Aliyasema hayo akiwa NHC Makao Makuu Kambarage House jijini Dar es Salaam jana alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa Shirika. Hiyo ilikuwa ni siku yake ya pili ya ziara aliyoifanya katika shirika hilo lengo likiwa ni kukutana na baadhi ya wadau wanaofanya biashara na NHC.

"Ninawapongeza kwa kazi nzuri mnazozifanya, Wizara tunawaamini na tunawathamini, tunachotaka sasa ni kwa Shirika kusomeka ndani na nje ya mipaka kwa kazi zake nzuri kwani kama nchi, tuna Balozi takribani 70, tumepewa ardhi huko na Balozi zetu hazina majengo, fanyieni kazi hili muweze kujenga nyumba hadi huko Uingereza na Marekani muwe `the best in the World not only in Africa," alisema akimaanishakuwa shirika liwe zuri zaidi siyo tu Afrika, bali pia duniani,"

Alisema serikali inamiliki viwanja katika nchi tofauti ambavyo Tanzania ilipewa kwa ajili ya ujenzi, ila bado havijajengwa na kwamba hiyo ni fursa kwa Shirika kwani iwapo Wizara ya Ardhi itaingia katika makubaliano na Wizara ya Mambo ya Nje, viwanja hivyo vitahitaji wawekezaji na wajenzi na hii itakuwa nafasi nzuri kwa NHC kutekeleza majukumu hayo kwani Shirika lina uwezo na lina nia ya kuzidi kukua.

Aliwaasa wafanyakazi kuzidi kuwajibika ili kutambulika kimataifa akiahidi kulisaidia Shirika kadiri ya uwezo wake akiwa kama mlezi wake.

Aidha, aliwataka watumishi wa NHC kubadilika kifikra na kuwa na fikra za kibiashara zaidi kwa kutoa huduma za kuridhisha wateja na kutimiza utekelezaji wa miradi iliyoanzishwa kwa wakati.

"Nawapongeza sana kwa kazi kubwa mnayofanya katika Shirika licha ya kukabiliana na changamoto kama vile ugonjwa wa Corona" alisema.

"Ningependa NHC isomeke nje na ndani ya Tanzania kwani shirika hili limemudu kudumu katika utendaji tangu mwaka 1961 lilipoundwa" alisema Pinda.

Aidha, alilielekeza Shirika kuzalisha zaidi kuliko kufanya kazi kikiritimba kwani Rais wa Awamu ya Sita, Dk.Samia Suluhu Hassan, ana maono.

Hivyo alilihamasisha Shirika liwe la kisasa zaidi kwa kufanya uwekezaji hususani nje ya nchi ili kuondoa madhila kwa Watanzania hasa wa hali ya chini.

"Hamuwezi kuendelea vizuri bila kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kwani mna Mkurugenzi Mkuu imara sana na mna rasilimali za kutosha. Nataka maslahi bora kwa wafanyakazi ili kusudi ndoto na mawazo mazuri yanayotolewa na waunda sera, yabadilike kuwa utendaji halisi, tuwe na nyumba nyingi zitakazoweza kuwahifadhi Watanzania wengi zaidi," alisema. Alisema serikali italisimamia vyema Shirika na kuhakikisha wanaondoa vikwazo vyote vinavyoonekana kuzorotesha biashara ya nyumba na kusaidia kupata maeneo ya uwekezaji na kuwezesha kukamilishwa kwa miradi iliyokuwa imesimama kwani Rais anataka mabadiliko kila nyanja inayoigusa jamii. Naye Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah Hamad, aliahidi kutekeleza kwa kazi maono hayo ya Rais ambayo yanasimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Waziri na Naibu wake. Hamad pia aliishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa miongozo yake madhubuti na ushirikiano wa mara kwa mara inayoutoa kwa Shirika katika hatua mbalimbali za maendeleo ya NHC.


# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



### Wafanyabiashara kupandisha holela bidhaa Mwezi Mtukufu

**BAADHI ya wafanyabiashara katika maeneo mbalimbali ya majiji na miji nchini, wanautumia Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan kupandisha bidhaa. Wanatumia fursa ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kuchuma kupitia kwa wananchi bila kujali kwamba, kitendo hicho ni kiovu na hakimpendezi Mwenyezi Mungu. Katika hali ya kawaida, tulitarajia kwamba wafanyabiashara hao wangeutumia muda huu, kutenda mema kwa kuuza kihalali bidhaa zao husus an zinazotumika zaidi na wafungaji badala ya kuwalangua**




## MAONI YA MHARIRI

### Wafanyabiashara kuweni waungwana Mwezi Mtukufu

WAISLAMU kote nchini kama ilivyo kwa wenzao sehemu nyingine duniani, walianza Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan wiki iliyopita.

Ni kipindi cha takriban mwezi mmoja ambacho ndugu zetu wa Kiislamu hufunga.

Mfungo wa mwaka huu kwa Waislamu, umekuja sambamba na Kwaresma kwa upande wa ndugu zetu Wakristo, ambapo nao kwa mujibu wa imani yao, hutakiwa kufunga katika kipindi kisichopungua siku 40.

Wakati Wakristo wakiwa wamebakiza takriban wiki moja na ushee kuikamilisha Kwaresma, Waislamu kwa upande wao, ndiyo kwanza wana wiki moja na ushee tu tangu wauanze Mwezi wa Ramadhan.

Lakini ni jambo la kusitikisha kuona kwamba wakati waumini wa madhehebu hayo wakiwa katika hali hiyo, wapo baadhi ya wafanyabiashara wenye tamaa ambao hutaka kukitumia kipindi hicho kuvuna utajiri badala ya kutafuta thawabu kwa Mungu.

Kipindi cha Kwaresma na Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, watu hutakiwa kufanya matendo mema na kujizuia na aina yoyote ya dhuluma.

Ni mbaya na haistahili kwa baadhi ya wafanyabiashara, kuvitumia vipindi hivi vitakatifu kujinufaisha.

Ni muhimu basi kwa wafanyabiashara wote kufanya biashara zao kwa kuzingatia kutopata hasara wala kutaka kupata faida kubwa.

Mathalani, utakuta katika baadhi ya masoko jijini Dar es Salaam na masoko mengine mijini, muhogo mmoja uliokuwa ukiuzwa Sh. 500 kabla ya Mfungo, hivi sasa unauzwa kati ya Sh. 1,000 na Sh. 1,500.

Kadhalika, magimbi kabla ya Waislamu kuanza Mfungo, gimbi moja liliuzwa kwa kati ya Sh. 300 na Sh. 500, lakini hivi sasa linauzwa kati ya Sh. 1,000 na 1,500.

Tunawasihi wafanyabiashara wenye tabia ya kupandisha bei ya bidhaa muhimu zinazotumiwa na wafungaji, waache kwani kufanya hivyo ni kuwatesa waumini wenzenu.

UMGL MEDIA Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255693257410 / 0766005061 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255713055011 / 0621350860 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** jaridalamwekeleo@gmail.com |




Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
godfreysanga774@yahoo.com

# Wanaotiririsha majitaka wakati wa mvua washughulikiwe

KILA mmoja anajua vema umuhimu mkubwa wa uwepo wa mvua katika maisha ya kiumbe chochote chini ya jua.

Ninapozungumzia mvua, hapana shaka wakulima katika maeneo mbalimbali ya nchi, wananielewa kwa haraka kuhusu manufaa yake na huenda si kwa wakulima tu, bali pia hata kwa wavuvi na wafugaji.

Lakini yote kwa yote, kila kiumbe mvua ina umuhimu na hasara endapo ikizidi.

Kwa mujibu wa wanajiografia, mvua ni matokeo ya mawingu yaliyopo angani kuyeyuka na hii ni baada ya mvuke uliotoka katika rasilimali misitu, mabwawa, vijito na bahari.

Hata hivyo, licha ya umuhimu na faida ya uwepo wa mvua, baadhi ya watu huitumia vibaya pindi inaponyesha kwa kuzibua vyoo na kuruhusu majitaka kutiririka bila kujali kama yanaelekea kwenye makazi ya watu au la.

Jambo hili halikubaliki hata kidogo kwani ni hatari kwa afya ya jamii na viumbe vingine vingi kwani milipuko mingi ya magonjwa huanzia hapo ikiwemo kuhara, kipindupindu hata U.T.I.

Je, wanaofanya hivyo, ina maana hawajui hatua wanazoweza kuchukuliwa kwa kukiuka sheria ya utunzaji wa mazingira?

Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, vyombo hivi vimekuwa vikiendelea kutoa elimu kwa jamii ya namna ya uhifadhi na njia sahihi ya vitu hatarishi hapa nchini.

Nafikiri unaweza kuungana na wazo langu kwamba sheria na faini ziongezwe kwa yeyote atakayebainika kufanya vitendo hivyo na ikiwezekana washughulikiwe kwa mujibu wa sheria ya utunzaji wa mazingira ili iwe mfano kwa wengine.

> **Jambo hili halikubaliki hata kidogo kwani ni hatari kwa afya ya jamii na viumbe vingine vingi kwani milipuko mingi ya magonjwa huanzia hapo ikiwemo kuhara, kipindupindu hata U.T.I....**

Tangu enzi, tumesoma na kusikia kuwa, mazingira ni kitu chochote kinachotuzunguka. Ina maana kwamba, hata mimi na wewe ni mazingira, tukichafua mazingira, tumejichafua wenyewe.

Nalazimika kuamini kwamba wale wanaochafua mazingira kwa njia hii ama nyingine, wanaijaribu sheria.

Tuungane pamoja kutunza mazingira ili tupate mvua nyingi na kuwa salama kiafya kuitangaza nchi yetu katika ramani ya dunia.

# Maafisa kilimo Ruangwa wakabidhiwa pikipiki 53

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

SERIKALI wilayani Ruangwa, imesema itaanza kupima uwezo walionao maafisa ugani kwa kuangalia mafanikio katika uzalishaji wa mazao mbalimbali wilayani humo.

Sambamba na hilo, imesema uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita uoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, hautawavumilia maafisa wanaofanya kazi kwa mazoea badala ya matokeo chanya.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Hassan Ngoma, wakati akikabidhi pikipiki 53 kwa maafisa kilimo ngazi ya viijiji na kata wa halamshauri ya wilaya hiyo, juzi.

Pikipiki hizo zilimetolewa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuimarisha huduma za ugani ili ziwafikie wakulima kwa wakati mashambani.

Tukio la makabidhiano hayo lilifanyika katika ghala la kuhifadhia mazao la Lipande nje kidogo ya mji wa Ruangwa, ambapo DC Ngoma aliwataka maafisa hao kuhakikisha wanabadili matokeo ya uzalishaji kwa wakulima baada ya kupokea nyenzo hizo.

"Nataka tuwekeane malengo ambayo tutayapima na yapimike. Haiwezekani uzalishaji ukabaki kama ulivyo sasa au kushuka zaidi kipindi hakukuwa na nyezo kwa wataalam wetu, na sasa ambapo tunawapa pikipiki hizi," alisema.

DC Ngoma alisema anatarajia kuona maafisa kilimo kote wilayani, wanasambaa vijijini hasa katika maeneo ya mashamba kuangalia muenendo wa uzalishaji wa mazao, hasa ikizingatiwa taifa limepitia katika kipindi kigumu

**Pamoja na mambo mengine, ziara hiyo ilikuwa na lengo la kukagua uhai na utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025.**



Mmoja kati maafisa ugani akikabidhiwa pikipiki

## Wanawake watakiwa kuwakagua watoto

**Na Claudia Kayombo, Singida**

WANAWAKE nchini, wamehimizwa kuwa karibu na kufuatilia mienendo ya watoto wao ili kuwalinda dhidi ya vitendo vya unyanyasaji.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Idara ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika Jimbo Kuu la Kanisa Katoliki la Arusha, Padri Denis Ngowi, alipokuwa akizungumza na waumini wa kanisa hilo Jimboni Singida. Padri Ngowi alikuwa akizungumza baada kuadhimisha Ibada ya Misa Takatifu ya Dominika ya Tano ya Kwaresma katika Kanisa Kuu la Kiaskofu la Moyo Mtakatifu wa Yesu.

Alisema kufuatilia mienendo ya watoto na kuwachunguza, kutasaidia kubaini haraka kama wanafanyiwa vitendo vya ukatili hasa wakati huu uliokithiri kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kina mama, wakagueni na kuwalinda watoto badala ya kuwaandalia kwa chakula pekee, fuatilieni elimu wanayopewa watoto. Siogopi kueleza haya kwa sababu dunia imefika ilipo," alisema Padri Ngowi.

Kiongozi huyo wa kidini, alisema malezi na makuzi ya mtoto katika dunia ya sasa, yamepoteza misingi na matokeo yake, ni watoto kujilea wenyewe wakati wazazi wakijikita katika utafutaji wa fedha.

Alisema jambo la kutia uchungu zaidi ni kuona akina mama ambao ni wahusika wakubwa katika kuwalea watoto duniani, wamekuwa ndiyo vinara wa ukatili.

Padri Ngowi alitoa mfano wa mtoto aliyeuawa kwa kuteswa na kisha kupigwa kwa nyundo, kunakodaiwa kufanywa na baba yake mkoani Arusha, kuwa mama wa kambo ndiye aliyemchochea baba huyo kutekeleza ukatili huo usiovumilika.

"Ninyi kina mama wenye matumbo ya uchungu, mnayapeleka wapi matumbo yenu," alisema kwa hisia za kusikitishwa na ukatili dhidi ya mtoto.

Pia alionya tabia ya baadhi ya kina mama kuwaeleza watoto changamoto za tabia zinazofanywa na baba zao kuwa hazijengi familia yenye maadili bali ya uhasama. Alisema Kanisa linamlinda mtoto kwa kuwa ni zawadi kutoka kwa Mungu. "Kanisa linamlinda mtoto katika namna tatu, ya kwanza tangu kutungwa mimba ambapo usalama wa mtoto unakuwa mikononi mwa baba na mama.

## ...Wakulima 'walilia' mikopo ya matrekta

**Na Mwandishi Wetu, Bagamoyo**

WAKAZI wa Kijiji cha Matipwili wilayani Bagamoyo, wameiomba serikali iwape elimu kuhusu namna ya kupata mikopo ya matrekta ili yasaidie kuboresha shughuli za kilimo.

Kadhalika, wananchi hao pia wametaka kumalizwa haraka kwa mradi wa maji unaotekelezwa katika kijiji hicho na Kampuni ya Ibla Contract, uliogharimu Sh. milioni 700 ili waanze kunufaika na huduma za maji.

Wakizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni kwa niaba ya wenzao, Neema Kipindura na Jumanne Ally, walisema watu wengi katika kijiji hicho wanajihusisha na kilimo na uvuvi mdogo mdogo katika Mto Wami. Walisema hata hivyo, shughuli hizo hazina tija kwa sababu wanazifanya kwa kutumia zana duni na kwamba wakati umefika wa serikali kuwaelekeza namna ya kupata mikopo ya matreketa kwa ajili ya kilimo na zana bora za uvuvi.

"Pamoja na kwamba tuna bahati ya kuwa na bonde linalofaa kwa kilimo, lakini tunashindwa kufikia malengo kwa sababu tunatumia jembe la mkono, kwa hiyo tunaiomba serikali itusaidie namna ya kupata mikopo ya matrekta," alisema Neema. Kwa upande wake, Ally aligusia mradi wa maji ambao alisema ingawa umefikia hatua nzuri, lakini bado unasuasua kukamilika na kusababisha wananchi kuendelea kukabiliwa na kero ya huduma za maji.

"Wananchi tunalazima kwenda Mto Wami kuchota maji, hali inayosababisha baadhi yetu kuliwa au kujeruhiwa na mamba. Haya yote yanatokana na kusuasua kwa mradi wa maji ambao mabomba yameshasambazwa mitaani," alisema Ally. Akizungumzia changamoto hizo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Msikitini, Alawi Abeid, alikiri kuhusu tatizo la wananchi kukosa zana bora za kilimo ambazo zingewasaidia kuboreshga shughuli zao.

Pia alizungumzia kwa kifupi tatizo la kutokamilika kwa mradi wa maji

"Nikianzia kilimo katika kijiji chetu, ni kweli kwamba tuna ekari 500, lakini kwa sababu ya kukosa matrekta, tulitumia asilimia 20 tu ya eneo hilo. Tunashindwa kuzalisha mazao kwa wingi kwa sababu tunalima kwa jembe la mkono," alisema Abeid. Akizungumzia mradi wa maji, alisema umefikia hatua nzuri, lakini umesimama kwa muda mrefu na hakuna sababu inayotolewa na wahusika.

Kiongozi huyo wa kijiji alisema hali hiyo inawalazimisha wananchi kwenda Mto Wami kuchota maji kwa matumizi mbalimbali, jambo linalotishia maisha yao.

# Waomba sekondari ya watu wenye ulemavu

**Na Lauden Mwambona , Mbozi**

SERIKALI imeombwa kuanzisha shule ya sekondari ya wenye ulemavu mkoani Songwe ili wanafunzi wa aina hiyo wanufaike na kufikia ndoto zao.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu Maalumu katika Shule ya Msingi Mwenge ya Mbozi mkoani Songwe, Eden Ngogo ambaye pia ni mwenye ulemavu wa macho, alitoa ombi hilo mbele ya Wakuu wa Idara za Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi (CMT) waliotembelea kitengo hicho.

Ngogo alisema ni muhimu kuanzisha sekondari ya wenye ulemavu ili kuendelea kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu wayafikie malengo yao.

Awali, mwalimu wa wanafunzi wasioona, Revina Kayombo, aliishukuru Halmashauri ya Wilaya kuanzisha kitengo cha wanafunzi wenye ulemavu wa akili ambacho kinawasaidia kujifunza ufundi baada ya kumaliza elimu ya msingi kama hawajachaguliwa kujiunga na sekondari.

> **Jitihada mbalimbali za kuimarisha ubora wa mafunzo, zimefanyika kupitia uhuishaji wa mitaala ya kufundishia pamoja na ununuzi wa mitambo...**

Hata hivyo, Kayombo alitaja changamoto wanazokutana nazo kuwa ni ukosefu wa kisima cha maji ya kudumu, choo maalumu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo na uzio wa bweni la kike.

Nyingine ni uhaba wa vyumba vya madarasa, bwalo la chakula, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, upungufu wa walimu, vifaa vya michezo, maktaba, samani na uwanja wa michezo. Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Oscar Mgani, aliwapongeza walimu wa shule hiyo hasa Kitengo cha Elimu Maalumu kwa kuwafundisha na kuwahudumia wanafunzi hao.



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohammed Said Mohammed (Dimwa - aliyevaa koti jeusi na kanzu nyeupe), akiwa na viongozi mbalimbali wa Chama wakati akizindua jiwe la msingi la kisima cha maji safi na salama katika Shehia ya Mzambarauni Jimbo la Chumbuni, Zanzibar juzi. Picha: (Mpigapicha Wetu)

## Mil. 200/– zamwagwa Ruangwa zijenge madarasa 10

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, imetoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 10 katika Shule za Msingi Nandanga na Likunja wilayani humu.

Mbali na madarasa hayo 10, katika miradi hiyo pia zitajengwa ofisi nne za walimu, mbili katika kila shule.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Frank Chonya.

Chonya alikuwa akizungumza na wananchi wa vijiji hivyo kwenye mikutano ya hadhara iliyoandaliwa mahsusi kuwatangazia uwepo wa miradi hiyo ya kimkakati.

Katika mikutano hiyo, Mkurugenzi Chonya alisimamia uundwaji wa kamati za ujenzi ambazo zitasimamia shughuli za mradi mwanzo hadi mwisho.

Kijiji cha Nandanga kipo Kata ya Luchelegwa na Likunja kinapatikana Kata ya Likunja na kwamba ujenzi wa miradi hiyo umezilenga shule kongwe ambazo zina idadi kubwa ya wanafunzi kwa sasa.

Katika mikutano hiyo, Chonya aliongozana na Afisa Elimu ya Msingi, George Mbesigwa, na Mhandisi kutoka Idara ya Ujenzi wa Majengo, Mhandisi Noel.

## Majungu kwangu hayana nafasi – RAS mpya Singida

**Na Claudia Kayombo**

KATIBU Tawala mpya Mkoa wa Singida, Fatma Mganga, amewaonya wafanyakazi wa idara mbalimbali kuwa hayupo tayari kupokea majungu bali maoni yenye tija.

Mganga amesema kimsingi majungu katika maeneo ya kazi kwake hayana nafasi.

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya kumkaribisha rasmi kushika nafasi hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa wa Singida wiki iliyopita.

Mganga aliteuliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwa Ofisa Tawala wa Mkoa wa Singida hivi karibuni.

Kabla ya uteuzi huo, Mganga alikuwa Ofisa Tawala wa Mkoa wa Dodoma.

Aidha, alimuomba Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ampe ushirikiano kwani hatakuwa kikwazo kwake.

"Namshukuru Mungu kwa Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuniteua miongoni mwa Watanzania zaidi ya milioni 60 nije hapa Singida kama Ofisa Tawala wa Mkoa… Namshukuru sana kwa kuniona, nilikuwa Dodoma na sasa nipo hapa Singida.," alisema Mganga na kuongeza:

"Katibu Tawala kwa nafasi yake, ni mtendaji, naomba ushirikiano wako Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, naahidi sitakuwa kikwazo kwako, tushirikiane tufanye kazi vizuri Mkoa upo hivi kutokana na utendaji wenu mzuri."

Alifafanua: "Mimi kitaaluma ni daktari, niliwahi kuwa Mganga Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi na Ofisa Tawala Mkoa wa Dodoma, hivyo nitawapa ushirikiano ili kufanikisha yale ambayo Rais anataka yafanyike."

Aidha, aliwausia wafanyakazi mkoani hapa kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

Naye Ofisa Tawala aliyemaliza muda wake, Doroth Mwaruko, baada ya kuwashukuru idara mbalimbali za Mkoa kwa kufanya nao kazi vizuri, pia alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba kwa kumheshimu wakati wote.

Aliwataka wafanyakazi mkoani humu kufanya kazi kwa weledi kwani mafanikio ya Mkoa yanampa heshima Rais ambaye atazungumzwa vizuri kutokana na maendeleo ya maeneo husika.

"Watumishi wa umma kazi yetu ni kuwahudumia wananchi, ninyi ni sehemu ya mafanikio ya Mama Samia, anapozungumzwa vibaya, ni kwa sababu ya ninyi, hivyo fanyeni kazi aione ili Rais azidi kutukuka," alisema Doroth.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba alimkaribisha Katibu Tawala mpya mkoani humu na kumuahidi kumpa ushirikino wa kutosha.

"Wote ametuleta Rais, nitakupa ushirikiano, tufanye kazi kwa ufanisi, naombeni sana watumishi wenzangu wa idara Mbalimbali, tumpe ushirikiano, RAS wetu ni mpole, lakini anataka matokeo, mimi namfahamu vizuri," alisema Serukamba.

Akimzungumzia RAS mstaafu Doroth, Mkuu wa Mkoa alisema alikuwa kiongozi shupavu na hodari anayefuatilia mambo mengi serikalini na kuwezesha kutekelezwa kwa miradi mingi mkoani humu.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo
JARIDA
Jumatano Machi, 29-Aprili 4, 2023

# Jungu kuu




**Jarida hili haliuzwi**




# Dk. Samia alivyosambaza neema Singida



## Mkomazi yaweka mikakati kuvutia utalii mbwa mwitu

UK. 11

## Wakazi Songwe walilia barabara kufungua mkoa



UK. 14

## Utaliu



# Zifahamu kwa undani sifa, tabia na uwezo wa mnyama twiga

TWIGA ni miongoni mwa wanyama wenye mvuto mkubwa kutokana na uzuri na mambo kadhaa ambayo yanatokana na asili yake ikiwa ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ndiyo maana nchini Tanzania, humtumia mnyama huyu kama alama ya urithi na utambulisho wa Taifa.

Aidha, kwa kutambua hilo, hata baadhi ya mashirika au kampuni, hutumia picha ya mnyama huyu twiga kama utambulisho wa Taifa na hivyo kuzidi kuwavutia watalii wengi zaidi kuingia nchini na hivyo kuliongezea Taifa pato.

Moja ya mashirika ambayo hutumia picha ya twiga katika bidhaa zake (ndege), ni Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), ambalo hutoa huduma ndani ya nchi na nje ya nchi.

Twiga, ni mnyama aliyebeba sifa nyingi ukilinganinisha na wanyama wengine wanaopatikana hapa duniani. Miongoni mwa sifa hizo ni urefu kuliko wanyama wote duniani, miguu mirefu, shingo ndefu na ulimi mrefu.

Sifa nyingine za ziada za mnyama huyu anayeaminika kuwa na maringo kuliko wote, ni kuwa na pembe fupi zilizo butu, wakati huo huo mwili wake ukiwa na mabaka yenye rangi ya kahawia na njano na kuzungukwa na rangi ya maziwa.


Hata hivyo, twiga jike ana rangi ng'avu zaidi kuliko dume huku twiga dume ni mkubwa na mzito zaidi kuliko jike.

Inaelezwa kuwa twiga aliyekomaa, ana urefu wa kati ya mita 4.8 na 5.5 na uzito wake ni kati ya kilo 700 na 1,500.

Urefu wa ulimi wake ni kati ya sentimita 46 hadi 50, wakati urefu wa moyo ni mita 0.6. Ana uwezo wa kukimbia kilomita 55 kwa saa. Mkia wake ambao ni meta 2.4 ni mrefu kuliko mikia ya wanyama wote duniani.

Mnyama huyu anapatikana katika nyika hususani sehemu zenye miti aina ya migunga pamoja na mikakaya kwani ndiyo miti ambayo huifurahia kwa sababu ndicho chakula chake kikuu.

Twiga hana ushindani mkubwa wa chakula na wanyama wengine kwa vile yeye hula majani ya juu ambayo wanyama wengine hawayafikii kwas urahisi.



### UZAZI NA MZUNGUKO WA MAISHA

Twiga hubeba mimba kwa siku 400 hadi 460 sawa na miezi 14 hadi 15, ambapo mara nyingi huzaa ndama mmoja, huku mapacha ikiwa ni mara chache.

Huzaa akiwa amesimama na kondo lake hukatika mara moja mtoto aangukapo ardhini tofauti na wanyama wengine kama ng'ombe ambapo huchukua saa kadhaa kondo kudondoka chini.

Ndama wa twiga aliyezaliwa, huwa na urefu wa mita 1.8 na uzito wa kuanzia kilo 40 hadi 70 na baada ya saa kadhaa, `mama' yaani twiga aliyezaa, ana uwezo wa kukimbia ndani ya wiki mbili za mwanzo, lakini ndama hutumia muda mwingi kujilaza chini huku akilindwa na mama yake kutokana tishio la simba, chui, fisi au mbwa mwitu.

> **Wanyama hawa wanachangamoto kubwa katika maisha yao wawapo porini kwani ni asilimia 25 hadi 50 ya maisha yao...**

Wanyama hawa wanachangamoto kubwa katika maisha yao wawapo porini kwani ni asilimia 25 hadi 50 ya maisha yao, huishia kati ya miaka 20 hadi 25 kwa twiga wa mwituni na miaka 28 wanaofugwa au kuishi nje ya mbuga.

Kuna nadharia inayoonyesha kuwa, twiga wana uhusiano na mnyama tandala, lakini zaidi wamejumuishwa kwenye jamii nyingine ya mnyama okapi anayepatikana nchi za Amerika, Nigeria na Afrika Kusini.

Utafiti wa mwaka 1920, ulithibitisha kuwa twiga hawachangamani na twiga wasio wa kundi moja. Pia pindi dume anapotaka kumpanda jike, basi huchagua yeyote aliye katika kipindi cha joto kwenye kundi lolote.

Twiga dume hutambua twiga jike walio katika kipindi cha joto kwa kuonja ladha ya mkojo.

### SHINGO NA NADHARIA ZA MTAANI.

Shingo ndefu ya twiga, imeibua nadharia nyingi mtaani, ambapo wapo watu wanaodai urefu huo ulitokana na wanyama hao kutaka kuyafikia matawi ya juu ili kujipatia chakula wakati wa ushindani na wanyama wenzao walao majani.

Hata wakati fulani hapa nchini, mtu aliyekuwa na uwezo zaidi ndani ya jamii, alipewa sifa ya kuwa ni 'matawi' ya juu yaani mtu mwenye hadhi ya kipekee kuliko wengine wote wanaomzunguka, hususani wanawake warembo.

Lakini wapo wanaoamini kuwa shingo za wanyama hao zinatokana na desturi zao za kusuguana kwa kutumia shingo au madume wanaogombea himaya ya majike kutumia shingo kama silaha ya mapambano.

Kitendo cha kusuguana shingo kwa twiga, hufanywa kwa madhumuni mbalimbali, mojawapo ni kupigana vita kali ambapo mara nyingine huwa ni kwa ajili ya kutaka kuchukua himaya ya kundi la twiga majike.

Lakini pia kuna siri ambayo watu wengi hawajui kwanini twiga hususani madume hutumia muda mwingi kusuguana kwa kutumia shingo.

Hakika Mungu alipoumba viumbe vyake, kila kimojawapo amekiachia vitu ambavyo aghalabu ni vya tofauti na kipekee, kwani twiga dume aliyopo kwenye upweke, hushiriki zaidi zoezi la kusuguana shingo kwa lengo la kutengeneza mihemko na hisia kali za mapenzi, hali ambayo mara nyingi huwafikisha kwenye kilele cha mapenzi.

### MIGUU NA MIONDOKO

Mara nyingi wanyama hawa wawapo kwenye mazingira yao ya kawaida, hutembea kwa madaha na maringo, jambo amabalo ukichanganya na rangi ya miili yao, huvutia mno.

Hata hivyo, ikitokea maisha yao yanahatarishwa ikiwemo kutaka kuvamiwa na simba, wanyama hawa wana uwezo wa kukimbia kwa kasi kubwa hadi kufikia umbali wa kilomita 55 kwa saa.

Aidha, twiga huitumia miguu yake ya mbele iliyo mirefu kama silaha hatari ya kummaliza adui yeyote anayejaribu kuhatarisha maisha yake akiwemo Simba na wanyama wengine hatari.

Teke la mbele likipigwa linakuwa na nguvu kubwa ya kuweza hata kupasua taya na hata uti wa mgongo wa Simba, jambo ambalo limekuwa si rahisi kwa simba kuwawinda ingawa ndio mnyama pekee tishio kwa twiga.

### MFUMO WA MZUNGUKO WA DAMU.

Hapa ndipo pana miujiza ya Mungu, kwani huwezi kufikiria kirahisi kwamba ni kiasi gani damu ya TWIGA inaweza kusafirishwa kutoka kwenye moyo hadi kwenye ubongo kutokana na umbali uliopo kati ya viungo hivyo vinavyotenganishwa na shingo ndefu.

Lakini Twiga kawekewa mazingira ya aina yake ya kuhakikisha mfumo wa damu unafanyika bila tatizo lolote licha ya kuwa na maumbile tofauti na wanyama wengine ya kuwa na shingo ndefu inayotenganisha kichwa na moyo.

Kwa haraka, ukimwangalia twiga utahisi maumbile yake yanaweza kuwa shida katika mfumo wa kusafirisha damu kutokana na umbali kati ya kichwa na moyo, lakini Mungu amemuumba mnyama huyo katika mazingira yanayomwezesha jambo hilo kufanyika bila shida.

Kwanza moyo wa twiga unakadiriwa kuwa na uzito wa kilo 10 na urefu wa sentimeta 60, hivyo una uwezo wa kuzalisha mgandamizo wa damu mara mbili ukilinganisha na wanyama wengine.

Hali hii husaidia kuupa nguvu mfumo wa kusukuma damu kwenda kwenye ubongo ulio kwenye kichwa kwa kuwa huwa kipo mbali kutokana na urefu wa shingo yake.

Pia karibu na shingo ya mnyama huyo, kuna mfumo tata unaoumbwa kwa ajili ya kuminya damu hiyo kwenda kwa wingi kwenye ubongo pindi anapoinamisha shingo.


### MAAJABU YA USINGIZI WA TWIGA

Twiga ni miongoni mwa mamalia wanaolala muda mfupi zaidi kuliko wote ambapo hutumia wastani wa dakika 10 hadi saa mbili katika saa 24 za siku.

Twiga anaweza kula kilo 29 katika mlo wake kwa siku.

**Imeandaliwa na Godfrey Sanga kwa msaada wa Mitandao**

Utalii



# Mkomazi yaweka mikakati kuvutia utalii mbwa mwitu

**Na Mwandishi Wetu, Same**

HIFADHI ya Taifa ya Mkomazi, inajenga boma jipya la kuwatunza wanyama pori aina ya mbwa mwitu kuwawezesha watalii kuwaona kwa urahisi wanapotembelea hifadhi hiyo maarufu pia kwa wanyama pori aina ya faru weusi.

Boma hilo litakalojengwa eneo la Mbula, litawasaidia watalii wanaopenda kuwaona wanyama pori hao, kuwaona kwa urahisi kuliko katika hifadhi nyingine ambako wanyama pori hao huonekana kwa nadra.

Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, ndiyo hifadhi pekee nchini inayozalisha mbwa mwitu na kuwasambaza katika hifadhi nyingine za taifa zenye mifumo ya ikilojia inayofanana na hifadhi hiyo.

Pamoja na kuzalisha mbwa mwitu ambao ni wanyama pori walio katika hatari ya kutoweka duniani, boma hilo jipya, pia litakuwa sehemu ya kivutio cha watalii ambao watakuwa na nafasi ya kuwaona kwa urahisi wanyama pori hao kuliko ilivyo sasa.

> **Kutokana na asili yao, wanyama pori hawa hula nyama na hutembea kwa makundi na wakati mwingine huingia katika maeneo ya binadamu na kuua mifugo na ndipo wanapo uawa kwania ya kulipa kisasi...**

Kwa mujibu wa takwimu za watalii hifadhini hapo, utalii wa mbwa mwitu ni kivutio kikubwa kwa wageni kutoka nchi za Marekani, Uingereza, India na nchi nyinginezo na boma hilo litaongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi hiyo.

Tayari mbwa mwitu zaidi ya 300, wamezalishwa katika hifadhi hiyo na wamesambazwa katika maeneo mengine ya ikolojia ya Tsavo/Mkomazi ambayo imesambaa hadi katika nchi jirani ya Kenya.

Wengine wamesambazwa kwa makundi katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Pori la Akiba la Maswa.

Mhifadhi Mwandamizi katika hifadhi hiyo, Emmanuel Sizya, anasema uzalishaji wa mbwa mwitu, utasaidia kuongeza idadi ya wanyama pori hao ambao wako katika hatari ya kutoweka kutokana na sababu mbalimbali.

"Ni wanyama walio katika tishio la kutoweka duniani kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo magonjwa na shughuli za kibinadamu ambazo zina waathiri sana wanyama pori hao.

"Kutokana na asili yao, wanyama pori hawa hula nyama na hutembea kwa makundi na wakati mwingine huingia katika maeneo ya binadamu na kuua mifugo na ndipo wanapo uawa kwania ya kulipa kisasi, na hili limeathiri sana idadi yao hivyo ni muhimu kuwalinda, "anasisitiza Sizya.

Anaeleza faida ya wanyama pori hao kuwa ni pamoja na kuwa muhimu kiikolojia ambako huvutia watalii lakini pia ni wafanya usafi porini hasa wanapokutana na masalia ya wanyama wengine waliokufa au kuuawa na wenzao na kuleta uwiano wa asili katika hifadhi.

Akifafanua mikakati ya kuwalinda wanyama pori hao, Sizya anasema pamoja na kuongeza uzalishaji, pia wanaboresha vinasaba kwa kuunganisha na wengine walio katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Pori la Akiba la Loliondo ili kuwa na kizazi kinachohimili mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mradi wa kuwatunza mbwa mwitu, kwa mujibu wa Mhifadhi Sizya, ulianza hifadhini hapo mwaka 1995 kwa kuwa na mbwa 25 ambao hutunzwa hapo kwa miaka mitatu na kisha kuachiwa kwa makundi katika hifadhi na maeneo yenye ikolojia inayofanana na ya Mkomazi ili warudi katika maeneo yao ya asili.



Siasa

# Dk. Samia alivyosambaza n

**Na Mwandishi Wetu**

WENGI wenye macho wameona kazi nzuri iliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake.

Dk. Samia, kiongozi mchakapakazi mwenye upendo wa mama halisi, amejitahidi kuing'arisha nchi kwa mafanikio makubwa ya kijamii na kiuchumi.

Mkoa wa Singida wenye wakazi zaidi ya milioni mbili, pekee umeelezea namna kiongozi huyo alivyoupaisha na kuuongezea neema katika sekta ya afya, elimu, miundombinu ya barabara, madaraja, maji safi na salama ndani ya kipindi hicho.

Mkuu wa Mkoa huu, Peter Serukamba ndiye anayebainisha kazi nzuri aliyoifanya Dk. Samia katika wilaya tano za mkoa huo ambazo ni Singida, Ikungi, Mkalama, Iramba na Manyoni ndani ya kipindi hicho.

Mkoa huo pia una halmashauri zake saba ambazo ni Singida, Singida Manispaa, Manyoni, Itigi, Mkalama, Ikungi na Iramba ambazo nazo zimenufaika uongozi wa mama huyo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Serukamba anasema Dk Samia anataja namna Rais alivyousaidia mkoa huo kuwa ni




**Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akitoa taarifa ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka m Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa (NEC) Mkoa wa Singida, Yohana Msita na kulia ni Katibu Tawala Msaidizi eneo la Uza**

> **Bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri imeongezeka kutoka zaidi ya Sh. bilioni 16.89 mwaka 2020/2021 hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 22.4 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 33...**

pamoja na kuongeza bajeti ya sekretarieti ya mkoa na halmashauri zake.

Anasema katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa mama Samia, bajeti imeongezeka kutoka zaidi ya Sh bilioni 180.1 mwaka 2020/2021 hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 239.8 mwaka 2022/2023.

Serukamba anasema ongezeko hilo la asilimia 33.09 limesaidia kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi kwa kiwango kikubwa katika Mkoa wa Singida.

"Bajeti ya mapato ya ndani ya halmashauri imeongezeka kutoka zaidi ya Sh. bilioni 16.89 mwaka 2020/2021 hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 22.4 mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 33," anabainisha Serukamba.

Anasema serikali kuu imebainisha bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni 1.05 kwa mwaka 2023 kwa ajili ya kuwalipa madiwani posho, posho ya madaraka kwa watendaji wa kata, posho za mawasiliano kwa watendaji wa vijiji posho za kila mwezi badala ya fedha hizo kulipwa na halmashauri.

"Mpango huu wa serikali kuu kulipa waheshimiwa madiwani posho, watendaji wa kata na vijiji haujawahi kufanyika katika awamu zote zilizopita," anasisitiza Serukamba.

Mkuu huyo wa mkoa anasema zaidi ya sh. bilioni 1.48 zimetumika kujengea nyumba za makazi ya maofisa watatu waandamizi, ofisi ya madereva na nyumba tisa za maofisa tarafa.

Fedha nyingine zaidi ya sh. bilioni 2.85 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wakurugenzi katika halmashauri za Iramba na Singida.

**SEKTA YA AFYA**

Katika kipindi hicho sekta ya afya, imeimarika kwa kiasi kikubwa ambapo wananchi wamekuwa na uhakika wa kupata matibabu kwa kusogezewa huduma za afya jirani tofauti na ilivyokuwa awali.

"Katika hospitali ya rufaa ya mkoa zaidi ya Sh. bilioni 11.83 zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi, jengo la wagonjwa wa dharura, nyumba ya mtumishi, ununuzi wa vifaa tiba na ukarabati wa vyumba vya "CT- SCAN na Digital X-Ray, ujenzi wa jengo tengefu la sakafu nne na mafunzo kwa watumishi kwa huduma za EMD, ICU na CT scan," anasema mkuu huyo wa mkoa.

Serukamba anasema mkoa wake ulipokea sh. bilioni 6.65 kwa ajili ya kujenga hospitali nne za wilaya katika halmashauri za Ikungi, Mkalama, Singida na Itigi na ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni.

"Mkoa ulipokea zaidi ya sh. bilioni 8.9 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 20 kupitia fedha za tozo za miamala ya simu, Benki ya Dunia, ruzuku ya Serikali Kuu na mapato ya ndani," anasema.

Anajaka zahanati hizo kuwa ni pamoja na Ntuntu, Chibumagwa, Ilunda, Gumanga, Mandewa, Urugu, Kisiriri, Mwanduijembe, Iyumbu, Unyambwa, Sanza, Makuro, Makuru na Mtipa.

Aidha, Serukamba anasema sh. bilioni 2.05 zilipokelewa na kutumika katika

# eema Singida




iwili tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aingie madarakani. Kushoto ni Mjumbe wa lishaji na Uchumi Mkoa wa Singida, Stanslaus Choaji. (Picha: Mpigapicha Wetu)

ununuzi wa vifaa tiba kwenye hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati katika halmashauri za Iramba, Mkalama, Ikungi na Manyoni.

"Kwa ajili ya uhamasishaji wa chanjo ya UVIKO 19 wananchi 906,420 sawa na asilimia 102 kati ya walengwa 892,060 walipatiwa chanjo ambapo zaidi ya sh. bilioni 1.065 zilitumika katika mchakato huo ambapo mkoa wa Singida ulifanikiwa kufikia lengo la kitaifa," anasema.

**SEKTA YA ELIMU**

Katika kipindi cha miaka miwili ya kuelekea sera ya elimu bila malipo, mkoa umepokea zaidi ya sh. bilioni 16.04 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 809 vya madarasa katika shule shikizi, msingi na sekondari.

Mkoa pia umepokea zaidi ya sh. bilioni 2.8 za kugharimia hatua za mwisho za ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari.

Serukamba anasema hali kadhalika katika kipindi hicho, mkoa umepokea sh. bilioni 5.8 zilizotumika katikia ujenzi wa vyumba 290 vya madarasa ya kidato cha kwanza na kujenga shule mpya saba za sekondari.

**Kwa upande wa mtandao wa majitaka kwa sasa wakala imeanza kujenga mabwawa ya kutibu majitaka na baadaye upo mpango wa kujenga mitandao ya mabomba ya kukusanyia majitaka**

Mkuu huyo wa mkoa anasema hatua hiyo imewawezesha wanafunzi 1,510 kupunguza umbali wa kutembea mwendo mrefu wa kati ya kilomita 10 hadi 20 walizokuwa wakitembea kila siku kufuata shule.

"Mkoa wetu umepokea sh. bilioni 7.23 za ujenzi shule mpya tisa za sekondari za kata za sekondari za mkoa. Wanafunzi 1,612 wamepata nafasi katika shule hizo tisa, kwa hiyo wamepunguza tatizo la kutembea umbali mrefu kufuata shule," anasema Serukamba.

"Fedha nyingine sh. bilioni 1.27 zimepokelewa na kutumika katika kukarabati mabweni tisa na mabwalo mawili katika shule za msingi na sekondari.

Hali kadhalika,ujenzi wa mabweni mawili kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu," anasema Serukamba.

**SEKTA YA MAJI**

UPATIKANAJI wa huduma za haji wa maji mkoani Singida, umeongezeka kutoka wastani wa zaidi ya lita milioni 8.38 mwaka 2020/2021 hadi kufikia zaidi ya lita milioni 9.8 kwa siku mwaka 2022/2023.

"Ongezeko hilo la uzalishaji linatokana na kukamilika kwa miradi mipya yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 838.66," anasema Serukamba.

Wateja wa maji nao wameongezeka kutoka 14,186 mwaka 2020/2021 hadi 16,521 mwaka 20223 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.5.

Upotevu wa maji umepungua kutoka asilimia 36.6 mwaka 2020//2021 hadi kufikia asilimia 31.4 mwaka 2022/2023, wakati makusanyo ya maduhuli yameongezeka kutoka zaidi ya sh. bilioni 3.28 mwaka 2020/2021 hadi sh. bilioni 3.81 mwaka 2022/2023.

"Kwa upande wa mtandao wa majitaka kwa sasa wakala imeanza kujenga mabwawa ya kutibu majitaka na baadaye upo mpango wa kujenga mitandao ya mabomba ya kukusanyia majitaka kutoka majumbani kwenda kwenye mabwawa," anasema Serukamba.

Ametanabahisha kuwa upatikanaji wa majisafi umeongezeka kutoka asilimia 58 mwaka 2021/ hadi 80 mwaka 2022/2023 kwa halmashauri ya manispaa ya Singida huku Mamlaka ya Maji (Suwasa), imepatiwa jukumu la kutoa huduma nje ya eneo la manispaa na sasa itaanza kuhudumia maeneo ya miji ya Ikungu, Puma, Sepuka, Irisya, Makiungu, Njiapanda na Ilongelo.

"Suwasa imefanikiwa kufanya ununuzi wa mita za maji 20,000 kwa sh. bilioni 1.04 mabomba kwa shilingi bilioni 1.1 na viungio kwa sh. milioni 870," anatanabaihisha Serukamba.

Aidha,Serukamba anabainisha utekelezaji wa mradi wa miji 28 unaokwenda kuanza ambapo kwa manispaa ya Singida umetengewa dola za Marekani milioni 17 ambazo zitatumika kujenga matanki manne, kuchimba visima 12 na kuongeza mtandao wa kilomita 45 pamoja na kujenga pampu za maji Mwankonko, Ititi na Mungumaji.

Anasema upatikanaji maji vijijini kwa mkoa wa Singida umeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2020/2021 hadi 64 sawa na wakazi 955,131 waishio vijijini hadi mwezi Februari mwaka huu (2023).

Ofisi ya Suwasa imepokea zaidi ya sh. bilioni 21.75 katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021/2022 hadi Februari mwaka huu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijini.

Mwezi Januari mwaka huu, mkoa wa Singida kupitia fedha za UVIKO-19 ulipokea mtambo wa kuchimbia visima virefu ili kuhakikisha maeneo yote yasiyo na maji yanapata maji ambapo hadi Februari 28, 2023 visima 11 vilishachimbwa katika wilaya za Manyoni na Singida huku lengo ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 upatikanaji wa maji mijini unafikia zaidi ya asilimia 95 na zaidi ya 85 vijijini.

"Huduma ya maji imeboreshwa katika miji ya Kiomboi kutoka asilimia 30 mwaka 2020 hadi 65 mwaka huu na katika mji wa Manyoni kutoka asilimia 65 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 73.5 mwezi Februari 2023," anasema Serukamba.

Katika mwaka huu wa fedha Ruwasa inaendelea kukamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa maji ya Kintiku/ Lusilile ambao unatarajiwa kugharimu zaidi ya sh. bilioni 12 ambao utadumu zaidi vijiji 11 katika wilaya ya Manyoni ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba mwaka huu na kuwanufaisha watu 55,000.

**SEKTA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Hali ya barabara katika Mkoa wa Singida inaridhisha ambapo asilimia 69.6 zipo katika hali nzuri, asilimia 24.6 wastani na asilimia 5.8 zina hali mbaya.

Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), mkoani humu inahudumia kilomita 1,718.31 za barabara kuu na zile za mkoa na kilomita 490.30 katika hizo ni za lami na sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilimita 1,228.01 ni barabara za changarawe.

Serukamba anasema serikali imepanga kutumia sh. milioni 18.97 kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika mkoa wake na kwamba mikataba 37 ya kazi hiyo ilishasainiwa katika kipindi cha mwaka 2022/2023.

"Serikali imetenga zaidi ya Sh. milioni 7.2 kwa ajili ya matengenezo ya kilomita 393 ya barabara za lami, ujenzi na matengenezo ya kingo za madaraja 15," anasema.

Pia ujenzi wa kivuko cha watembea kwa miguu katika barabara ya Kintinku kupitia Singida hadi Malendi.

Kwa mujibu wa mkuu wa mkoa, miradi ya ujenzi wa madaraja ya mabwawa ya Kindai na Monangi pamoja na kunyanyua matuta katika barabara ya Iyumbu hadi Mgungira kupitia Mtunduru hadi Magereza.

Na ujenzi wa Daraja la Itagata katika Barabara ya Rungwa kupitia Itigi hadi Mkiwa na ujenzi wa daraja la Milai A katika barabara ya Shelui kupitia Senkenke, Tulya hadi Tyegelo na madaraja ya Kinyangiri katika barabara ya Igugunoshamba kupitia Nduguti hadi Gumanga na ujenzi wa barabara ya lami kilomita moja kutoka Ikungi kupitia Londoni hadi Kilimatinde.

Serukamba anawataka wakazi wa Singida na Watanzania kwa jumla waendelee kumuombea Rais Dk. Samia ili Mungu ampe afya njema na maisha marefu.

Uchumi







# Wakazi Songwe walilia barabara kufungua mkoa

**Na Lauden Mwambona, Songwe**

MACHI 18, mwaka huu, wakazi wa Mkoa wa Mbeya na mikoa jirani, walikusanyika jijini Mbeya kuadhimisha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Ilikuwa hafla kubwa ambapo viongozi mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliongozwa na Naibu Katibu Mkuu (Zanzibar), Mohamed Said Mohamed (Dimwa) aliyekuwa mgeni rasmi.

Mgeni rasmi ulipofika muda wake wa kuhutubia, alipanda jukwaani,lakini akatoa nafasi kwa Wakuu wa Mikoa ya Mbeya na Songwe, waeleze jinsi walivyopokea fedha za maendeleo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, anaeleza mkoa wake ulivyopokea fedha na zilivyotumika ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia kwenye sekta za utawala, afya, elimu barabara na mikopo kwa jamii.

Naibu Katibu Mkuu Dimwa, anatoa nafasi nyingine kwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Machael, azungumzie jinsi fedha zilivyotiririka mkoani mwake kipindi cha miaka miwili.

Dk. Michael anataja miradi mbalimbali ikiwamo ya kukamilika kwa barabara ya kutoka Mpemba wilayani Momba hadi Isongole wilayani Ileje.

Anataja mabilioni ya Shilingi yaliyoingia mkoani Songwe kwa ajili ya sekta mbalimbali zikiwamo za elimu, barabara, maji na kuwapokea walimu wapya 342.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar Dimwa anasimama na kuwaagiza wajumbe wa Halmashauri Kuuu ya CCM mikoa hiyo kushirikiana na viongozi wa CCM wa mikoa na wilaya kwenda kukagua miradi yote ili kujiridhisha.

Pia anatoa nafasi kwa wananchi waliofurika kwenye maadhimisho hayo wenye jambo ili waseme mbele yake.

Ndipo kijana wa kiume ananyoosha mikono yake miwili juu ili azungumze mbele ya mgeni rasmi na hatimaye anapewa nafasi.

Kijana huyo anajitambulisha kwa majina ya Msukwa B. Msukwa, kutoka Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe.

Msukwa anamweleza Naibu Katibu Mkuu kwamba ipo barabara ya kutoka Mlowo wilayani Mbozi hadi Kamsamba wilayani Momba ambayo ni muhimu kwa uchumi wa mkoa na Tanzania kwa jumla.




> **Hadi Novemba, mwaka jana, jumla ya zabuni 28 zenye thamani ya Sh. bilioi 10.318 za awamu ya kwanza, zilikamilika na walianza kazi...**

Msukwa anaiomba serikali ijenge barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Hoja hiyo inawiana na mkazi wa Kijiji cha Igamba wilayani Mbozi, Juma Mwazembe, ambaye alilieleza gazeti la UELEKEO kwamba eneo la Kamsamba ndilo linalozalisha mpunga kwa wingi mkoani Songwe.

Mkoa wa Songwe ni mmoja wa mikoa inayozalisha chakula kwa wingi kwani taarifa za Katibu Tawala Msaidizi, masuala ya kilimo mkoa huo, Vanscar Kulanga, zinaonyesha Kamsamba imewahi kuzalisha mpunga uliofikia tani 105,000 kwa mwaka mmoja na mkoa pia umewahi kuzalisha tani 605,000 za mahindi huku ukiwa wa pili kwa kuzalisha kahawa aina ya arabika nchini.

Mazao mengine yanayozalishwa mkoani Songwe ni maharage, mtama, karanga, viazi mviringo, viazi vitamu na mihogo mbali ya aina mbalimbali ya matunda.

Kwa mtazamo huo, suala la kuwapo kwa barabara bora, ni la msingi ili mazao yatolewe maeneo ya vijijini kwenda maeneo mengine ya nchi.

Mkoa wa Songwe ni kitinda mimba kwa mikoa yote 26 nchini. Mkoa huu ulianzishwa mwaka 2016 baada ya kumegwa kutoka kwenye Mkoa wa Mbeya na unaundwa na wilaya za Ileje, Momba, Songwe na Mbozi.

Kwa uchanga huo, Kamati ya Ushauri Mkoa, mara kadhaa wamezungumzia umuhimu wa kuzifungua barabara ndani ya mkoa na zile zinazounganisha mikoa mingine.

Hata hivyo, Kaimu Meneja Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Injinia Suleiman Bishanga, anasema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia, inautambua Mkoa wa Songwe na ina mkakati wa kuboresha barabara zote.

Injinia Bishanga anatoa mfano kwamba, mwaka wa fedha 2022/23, serikali imetumia fedha nyingi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu katika barabara mbalimbali za Mkoa wa Songwe na pia imetenga karibu Sh. bilioni 11.3 kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Tanroads Mkoa huo, inahudumia barabara zenye urefu wa zaidi ya kilomita 982 zikiwamo kilomita 233.63 za barabara kuu na kilomita 749.01 za mkoa.

Injinia Bishanga anasema hadi Novemba, mwaka jana, jumla ya zabuni 28 zenye thamani ya Sh. bilioi 10.318 za awamu ya kwanza, zilikamilika na walianza kazi

Awamu ya pili jumla ya zabuni 19 zilifanyiwa kazi zikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 3.5 na wakandarasi wapo kazini.

Kaimu Meneja huyo anasema serikali pia imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika barabara za kutoka Mlowo hadi Kamsamba yenye urefu wa kilomita 130 ili zitafutwe fedha za kujenga kwa kiwango cha lami.

Kaimu Meneja anasema serikali inaendelea kuzihudumia barabara zote za mkoa zikiwamo za Mlowo hadi Kamsamba na Chang'ombe Mkwajuni wilayani Songwe.

Pia imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa madaraja ya Magambo na Galula katika barabara ya mkoa ya Galula hadi Namkukwe na sasa serikali inatafuta fedha za kujenga.


Barabara nyingine zinazofanyiwa upembuzi yakinifu ni za Kasumulu – Katumba Songwe na kwamba sehemu ya kwanza ya Isongole - Isoko yenye urefu wa kilomita 52.5 imetengewa Sh. bilioni 5 kwa ujenzi

Barabara nyingine zinazotarajiwa kujengwa kwa lami ni ile ya kutoka Iyula - Nyimbili-Hasamba - Izilya hadi Itumba na ile ya Mahenje hadi Vwawa.

Kana kwamba haitoshi, serikali pia imetoa fedha nyingi kutengeneza na kukarabati barabara zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na mijini (Tarura). Tarura Mkoa wa Songwe inahudumia barabara zenye urefu wa kilomita 3,341.63 zikiwamo kilomita 20.326 za lami na kilomita 2,353 za udongo wakati kilomita 967.8 ni za changarawe.

Hata hivyo, Injinia Bishanga anasisitiza kwamba serikali inatambua barabara zote na inaendelea kuzihudumia.

Afya


Nguruwe

# Historia ya gonjwa la Marburg, dalili na jinsi ya kujikinga nalo

MARBURG ni ugonjwa uliobeba historia kubwa ndani na nje ya Bara la Afrika na dunia kwa jumla.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), virusi vya Marburg ambavyo ni sawa na virusi hatari vya Ebola, viligunduliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1967 huko Marburg na Frankfurt nchini Ujerumani na Belgrade huko Serbia.

Baada ya kugundulika kwa ugonjwa huo kwa mara ya kwanza, watu 31 waliambukizwa virusi hivyo na saba kati yao, walifariki dunia.

Kwa mara ya kwanza, ugonjwa huo umegundulika nchini Tanzania katika Mkoa wa Kagera na watu wanane wameambukizwa ambapo watano kati yao, wamefariki dunia.


Tumbili

Waziri wa Afya wa Tanzania, Ummy Mwalimu, Machi 21, mwaka huu, aliutangazia umma na dunia kwa ujumla kuwa ugonjwa huo, tayari umeingia hapa nchini katika Mkoa wa Kagera na kusababisha madhara hayo.

Hata hivyo, kuna uwezekano mkubwa wa kupambana na virusi vya ugonjwa wa Marburg usiendelee kuenea hapa nchini kwa kuzitambua dalili zake.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam Machi 21, mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy aliwaondoa hofu Watanzania kwa kusema kuwa serikali imefanikiwa kuudhibiti ugonjwa huo usiendelee kuenea nje ya Mkoa wa Kagera. Kabla ya serikali kuthibitisha juu ya ugonjwa huo, ilizuka sintofahamu kubwa juu ya vifo hivyo kutokana na kutojulikana kwa gonjwa hilo na baadhi waliuhusisha na gonjwa hatari la Ebola ulioua maelfu ya watu katika nchi nyingi za Afrika zikiwemo Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC.)


Popo

**JINSI UNAVYOAMBUKIZA**

Marburg ni ugonjwa unaoambukizwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa njia ya kugusana au kutoka kwa mnyama kwenda kwa binadamu,

Kadhalika, huenea zaidi kupitia maji maji yatokayo mwilini kama damu, mbegu za kiume ambazo zinaweza kuwaambukiza watu wengine kwa miezi mingi baadaye.

Huu ni ugonjwa mwingine hatari wa mlipuko kama yanavyoripotiwa magonjwa mengine ya mlipuko yasiyo na tiba ya moja kwa moja kama Ebola.

**DALILI ZA MARBURG**

Dalili za awali za ugonjwa huo ni pamoja na homa, kichwa kuuma sana, misuli kuuma, kikohozi, maumivu ya viungo, kuumwa tumbo, kuhara, kichefuchefu na kutapika na upungufu wa damu katika mwili na hatima yake ni kifo.

Baadhi ya watu hutokwa na damu sehemu mbalimbali za mwili na kufa siku nane hadi tisa baada ya kuugua kwa sababu ya kupoteza damu nyingi.

Kwa wastani, virusi huua nusu ya walioambukizwa, lakini kwa mujibu wa WHO, aina hatari zaidi imeua hadi asilimia 88,

**VIRUSI VILITOKA WAPI?**

Kwa taarifa za wataalamu wa WHO, virusi vya Marburg vilipatikana kwa mara ya kwanza kwa tumbili wa kijani kibichi. Virusi hivyo pia vinahusishwa kupatikana kwa wanyama wengine wakiwemo popo ambao kwa Afrika, hupatikana kwa wingi nchini Uganda, DRC na Gabon.

Inaelezwa kuwa mara nyingi watu wanaoathirika zaidi ni wale wanaokaa muda mrefu kwenye mapango ya migodi yeye popo wengi.

**ULIVYOINGIA AFRIKA**

Nchi kadhaa za Afrika zimewahi kuripotiwa kukumbwa na mlipuko wa virusi hivyo zikiwemo DRC, Kenya, Afrika Kusini, Uganda na Zimbabwe.

Mlipuko wa mwaka 2005 nchini Angola, ulisababisha vifo vya watu zaidi ya 300. Lakini barani Ulaya, ni mtu mmoja tu alifariki dunia katika kipindi cha miaka 40 na mwingine mmoja nchini Marekani baada ya kurejea kutoka katika safari ya kuzuru mapango nchini Uganda.

**MILIPUKO MIKUBWA**

Kwa mujibu wa taarifa za WHO, mwaka 2017, Uganda uliua watu watatu na mwaka 2012, viliripotiwa visa 15 na watu wanne walifariki dunia.

Mwaka 2005, Angola kuliripotiwa visa 374 ambapo watu 329 walifariki dunia.

Mwaka 1998 hadi 2000, DRC viliripotiwa visa 154 ambapo watu 128 walifariki dunia.

Mwaka 1967, Ujerumani kuliripotiwa visa 29 na saba kati yao waliaga dunia.

WHO inazidi kufafanua kuwa, popo wa matunda wa rousette wa Misri, ndiye anayeaminika kuwa ni muenezaji mkuu wa virusi vya ugonjwa huo.

Popo wa matunda ya rousette, huwa na virusi. Aidha, nyani wa kijani kibichi na nguruwe, pia wanaweza kubeba virusi hivyo.

**Dalili za awali za ugonjwa huo ni pamoja na homa, kichwa kuuma sana, misuli kuuma, kikohozi, maumivu ya viungo, kuumwa tumbo, kuhara, kichefuchefu na kutapika...**

**JE, MARBURG INATIBIKA?**

Virusi vya ugonjwa huu unatajwa kutokuwa na tiba isipokuwa mgonjwa hutibiwa kwa dalili husika alizokuwa nazo.

Kadhalika, inaelezwa kuwa ugonjwa huu hauna chanjo maalum au matibabu ya virusi. Lakini, WHO inasema kwamba juhudi zinafanyika za kutengeneza aina mbalimbali za bidhaa za damu, dawa za kulevya na matibabu ya kinga,

Madaktari wanaweza kutoa maji mengi kwa njia ya dripu kwa mgonjwa aliyepoteza damu nyingi ili yachukue nafasi ya damu iliyopotea.

**JINSI YA KUJIKINGA NA MARBURG**

Watu kuepuka kula au kushika nyama za porini, kuepuka kuwa karibu na nguruwe katika maeneo yenye mlipuko,

Hali kadhalika, inashauriwa kwa wanaume waliowahi kupata virusi vya ugonjwa huu, kutumia kondomu kwa muda wa mwaka mmoja tangu kupata dalili au mpaka pale wataalamu wa afya watakapothibitisha mara mbili tofauti kwa kupima mbegu zao za kiume.

Vile vile, inashauriwa kwa wale wanaozika marehemu waliofariki dunia kwa ugonjwa huu, kuepuka kugusa mwili wake. Hata hivyo, kubwa zaidi, ni kuwahi matibabu haraka pindi dalili hizo zinapojitokeza.

**Na Godfrey Sanga kwa msaada wa Mitandao**

## Kilimo



# Tunda la parachichi na faida zake lukuki mwilini

UMAARUFU wa parachichi unatokana na umbile lake nyororo, laini na ladha isiyo ya kawaida.

Parachichi ni tunda ambalo ni la familia ya mdalasini na kuna aina kadhaa ya parachichi, kuanzia ukubwa, rangi na muundo.

Yote hukua katika asili ya hali ya hewa ya kitropiki na yanapovunwa ni nyororo na laini kama siagi ambapo yamekuwa maarufu katika kila kitu, kuanzia kwenye kuchanganyia katika mlo mpaka kula baada ya chakula.

Aidha, 80 ya gramu ya pachachichi, ina protini gram sita, Mafuta gram tano, wanga gram sita, potasiamu gram 360 na vitamin E gram 56.

**Faida 20 za kula parachichi**

1- Parachichi ni tunda la pekee ambalo limebeba virutubisho mbalimbali ambavyo ni muhimu kwa ajili ya miili yetu, baadhi ya virutubisho hivyo ni :-

- Kalori 240 (184 inatokana na mafuta)
- Miligram 11 za sodium
- Gram 13 za wanga
- Gram 10 za nyuzinyuzi za lishe
- Gram moja ya sukari
- Vitamin K asilima 26
- Vitamin C asilimia 17
- Potasiam asilimia 14
- Vitamin B5 asilimia 14
- Vitamin B6 asilimia 13
- Asidi ya folate asilimia 20
- Vitamin E asilimia 10

Virutubisho hivi ni muhimu kwa ajili ya mwili kujijenga na kujilinda dhidi ya magonjwa

2. Pamoja na parachichi kuwa na virutubisho mbalimbali, bado lina virutubisho muhimu tunavyohitaji kutoka kwenye mimea, virutubisho hivyo ni :-

.Corotenoids- Inapatikana kutoka kwenye parachichi na ina manuafaa makubwa kwa ajili ya miili yetu katika kulinda macho dhidi ya matatizo mbalimbali yakiwemo yale yatokanayo na umri.

-Persenones A na B- Hii huzuia uvimbe na saratani mwilini.

D-Mannoheptulose – Hii ni aina ya sukari inayopatikana kwenye parachichi na inaaminika kusaidia kutawala kiwango cha sukari mwilini.

3. Husaidia kupunguza uzito. Suala la kupunguza uzito linaathiriwa sana na mfumo mzima wa lishe, hivyo kula vyakula ambavyo vinawezesha mchakato wa metaboli kwenda vyema kutakuwezesha kupunguza uzito kwa muda mfupi.
Parachichi ni tunda zuri ambalo huwezesha mchakato wa metaboli kwenda vizuri mwilini.

4 Lina fetty acid
Fatty acid itokanayo na mafuta ya parachichi ambayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli mbalimbali katika miili yetu.
Fetty acid inahitajika katika uzalishaji wa homon, ukuaji wa seli pamoja na ufyonzwaji wa virutubisho.

> **Parachichi ni tunda zuri ambalo huwezesha mchakato wa metaboli kwenda vizuri mwilini...**

5. Hupunguza lehemu (cholesterol) mbaya.
Mafuta ya lehemu ni hatari ikiwa kiwango chake kitakuwa kingi mwilini, mafuta haya husababisha matatizo mbalimbali hasa maradhi ya moyo.
Matunda ya parachichi hayana lehemu mbaya inayoweza kuathiri afya.
Utafiti unaonesha kuwa watu wanaokula parachichi, kiwango chao cha lehemu mwilini ni tofauti na wale wasiokula kabisa.

6. Husaidia kukabili maradhi ya sukari
Parachichi ni tunda ambalo kiwango chake cha sukari hakina athari kwenye mwili.
Hivyo utumiaji wa parachichi utakuwezesha kuweka kiwango cha sukari kuwa katika hali nzuri ya wastani.

7. Hulinda afya ya moyo
Madini ya potasium yanapatikana kwenye tunda la parachichi kwa zaidi ya asilimia 14, ni muhimu sana katika utendaji kazi wa misuli ya moyo.

8. Huzuia uvimbe
Asidi ya Oleic inayopatikana kwenye parachichi, imebainishwa na wataalamu kuwa husaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia uvimbe mwilini.

9. Hulinda afya ya macho
Kemikali ya lutein na zeaxanthin, ni muhimu sana kwa ajili ya kulinda na kuimarisha afya ya macho.
Ikumbukwe kuwa parachichi ni tunda lenye kiasi kikubwa cha lutein ambayo pia hulinda macho dhidi ya matatizo mbalimbali yatokanayo na umri.

10. Lina potasiam nyingi kuliko ndizi
Watu wengi wanapenda ndizi kwa kuwa ni chanzo kimoja wapo cha madini ya potasium, lakini hawafahamu kuwa ndizi ina potasium asilimia 10 na parachichi ina asilimia 14, hivyo parachichi ni bora zaidi.
Potasium ni muhimu katika miili yetu kwani hutuwezesha kutawala kiwango cha sodium katika miili na kutuepusha na madhara yatokanayo na madini haya ya sodium.

11. Huboresha afya ya nywele na ngozi
Je, umewahi kusikia kuwa parachichi hutumika kutengenezea mafuta ya nywele na ya ngozi, hii ni kutokana na kushsheni vitamini E ambayo ni muhimu kwa ajili ya afya ya nywele na ngozi.
Hivyo, baadala ya kununua mafuta ya gharama kubwa ili kupata vitamin E kwa ajili ya ngozi na nywele, kula tunda la parachichi.

12. Huzuia saratani
Tafiti zilizofanyika zimebainisha kuwa kula matunda ya parachichi kunasaidia kupunguza kasi ya ukuaji wa seli za saratani ya tezi dume.
Hata hivyo, tafiti juu ya suala hili siyo nyingi sana, lakini bado unaweza kula parachichi na kupata faida nyingine nyingi.

13. Huimarisha mifupa
Kutokana na parachichi kuwa na vitamin K pamoja na madini ya kopa na folate ambavyo ni muhimu kwa ajili ya mifupa, tunda hili linakuwa na nafasi kubwa katika kuimarisha mifupa.

14. Huboresha mmeng'enyo wa chakula
Vyakula vyenye nyuzi nyuzi ni muhimu sana kwa ajili ya kufanya mmeng'enyo wa chakula uende vizuri.
Parachichi ni tunda lenye nyuzinyuzi kwa karibu asilimia 13 ambazo ni sawa na asilimia 54 unachotakiwa kula.

15. Ni muhimu kwa wajawazito
Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha folate, potassium, vitamin C na B6 ambazo ni muhimu kwa ajili ya afya na ukuaji wa mtoto, kunalifanya tunda hili kuwa na umuhimu mkubwa kwa wajawazito.
Hivyo inashauriwa wajawazito wazingatie ulaji wa matunda hasa tunda la parachichi.

16. Huimarisha kinga ya mwili
Kinga ya mwili hutegemea vitamini B, C na E ili kujiimarisha na kujijenga.
Hivyo ulaji wa parachichi utaimarisha kinga ya mwili kwani tunda hilo limesheheni vitamini hivyo.

17. Huboresha afya ya ubongo
Madini kopa yanayopatikana kwenye tunda hili kwa zaidi ya asilimia 19, yana nafasi kubwa katika kuufanya ubongo ufanye kazi vyema. Hivyo, ukitaka kuweka afya ya ubongo wako katika hali nzuri na kuweza kufikiri vyema, kula tunda la parachichi mara kwa mara.


18. Huboresha ufyonzaji wa virutubisho
Baadhi ya virutubisho hufyonzwa kunapokuwa na mafuta (fat soluble), virutubisho hivyo ni kama vile vya vitamin A, E,D na K, hivyo kula parachichi kutawezesha virutubisho hivi kufyonzwa vyema mwilini.

19. Humweka mtu katika hali nzuri
Baadhi ya tafiti zimeeleza kuwa watu wenye msongo wa mawazo, wana upungufu mkubwa wa madini ya potasium, kwa kuwa parachichi ni chanzo kikubwa cha madini hayo, basi tunda hili linaweza kusaidia sana kukuweka katika hali nzuri.

20. Huongeza nguvu mwilini
Miili yetu inategemea sana wanga, protin na mafuta ili kupata nguvu.
Hivyo, kuongeza parachichi katika mlo, kutawezesha kuuongezea nguvu mwilini.
Parachichi ni tunda linalopatikana kwa urahisi bila gharama kubwa ikilinganishwa na matunda mengine kama vile tofaa (apple) na kadhalika. Hivyo ni muhimu kuyafanya matunda kuwa sehemu ya mlo wako.

**Imeandaliwa na Mwandishi Wetu kwa msaada wa Mitandao.**

HABARIKUTOKA ZANZIBAR



# Dimwa afichua siri ili CCM iendelea kukubalika Z'bar

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said Mohamed (Dimwa), amesema ili CCM iendelee kukubalika na kuaminiwa na wananchi kupewa ridhaa ya kuongoza Zanzibar, kuna umuhimu mkubwa kwa viongozi wa chama hicho kuwa karibu na wananchi kwa kuwatembelea na kusikiliza kero zao.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kisima cha maji safi na salama kilichopo Mzambarauni, Shehia ya Karakara Jimbo la Chumbuni.

Kisima hicho kimechimbwa kwa ufadhili wa Mbunge wa jimbo hilo, Ussi Salum Pondeza. Aliserma, CCM inatambua kuwa huduma ya maji safi na salama, ni ya msingi kwa kila mkazi wa Zanzibar.

Dk. Dimwa alisema miradi mbalimbali imekuwa ikisainiwa chini ya Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa lengo la kuona wananchi wake wanapata huduma hiyo kila shehia.

Alisema katika miaka mitano ijayo, CCM inaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kutimiza azma ya ASP na CCM ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi katika maeneo ya vijijini na mijini inafikiwa. Sambamba na hayo, aliwataka Wabunge na Wawakilishi, kuhakikisha wanatekeleza ahadi walizozitoa wakati wa kampeni kwa vitendo ili kurejesha imani kwa wananchi katika kuiamini CCM kwenye kuleta maendeleo.

Aidha, alimttaka kiongozi huyo kuweka utaratibu mzuri wa kuona wananchi wake wanapata huduma zilizokuwa bora ikiwemo maji safi na salama hasa katika Mfungo Mtukufu wa Ramadhan.

> **Katika miaka mitano ijayo, CCM inaielekeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kutimiza azma...**

Naye Mbunge wa Jimbo la Chumbuni, Pondeza, alisema ujenzi wa kisima hicho ni utekelezaji wa Ilani ya CCM katika jimbo hilo, ambao mchakato aliuanza tangu mwaka 2008.

Alisema kisima hicho kiliharibika Aprili, 2022 na kusababisha wakazi wa jimbo hilo kukosa huduma ya maji safi na salama.

Mbunge huyo aliongeza kuwa kisima hicho kitawanufaisha wananchi wa shehia nne zilizopo katika jimbo hilo.

Alizitaja shehia zinaunda jimbo hilo kuwa ni Masumbani, Banko, Maruhubi na Karakana.

# Kortini akidaiwa kumchinja mtu shavuni na kidevuni

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

MKAZI Saateni visiwani hapa, Abdallah Said Hemed (25), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Mwanakwerekwe kujibu shitaka la kumchinja mwenzake kwa kisu kwenye shavu na kidevu.

Mshitakiwa huyo alisomewa shitaka lake hilo na Mwendesha Mashitaka, Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), Suleiman Fadhil, mbele ya Hakimu Nazrat Suleiman. Mwendesha Mashitaka Suleiman alidai kuwa mtuhumiw ahuyo alifanyakosa hilo Desemba 26, mwaka 2022 saa 4:30 asubuhi eneo la Malindi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo alimshambulia Khatibu Juma Abdallah, kwa kumrushia kisu na kumchinja sehemu ya shavu la kushoto na kidevu na kumsababishia maumivu mwilini mwake, kitendo ambacho ni kosa kisheria. Hata hivyo, mshtakiwa alikana shitaka hilo na kuiomba Mahakama impatie dhamana.

Upande wa mashitaka ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuiomba Mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasilisha mashahidi mahakamani.

Hakimu Nazrat alikubaliana na ombi la upande wa mashitaka na kuahirisha kesi hiyo hadi leo Jumatano.

Aidha, Hakimu Nazrat alimtaka mshtakiwa kujidhamini mwenyewe kwa Sh. 100,000 za maandishi pamoja na wadhamini wawili wenye Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.



Mbunge wa Jimbo la Chumbuni, Zanzibar, Ussi Salum Pondeza (wa pili kutoka kushoto), akitoa ufafanuzi kuhusu uchimbaji wa kisima cha maji safi na salama katika hafla iliyofanyika Mzambarauni, Shehia ya Karakara jimboni humo juzi. Wa kwanza kushoto, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) Picha: Mpigapicha Wetu).

# `Uhaulishaji ardhi uangaliwe upya'

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, imeshauriwa kuangalia upya utaratibu wa malipo ya uhaulishaji wa ardhi kwa kuweka miongozo mapema juu ya matumizi ya ardhi ili kuepusha usumbufu.

Wakizungumza katika kikao cha pamoja kati ya mawakili wasomi na uongozi wa wizara hiyo chini ya Waziri wa Ardhi, Rahma Kassim Ali, walisema mpango unaotumika sasa wa malipo unaleta usumbufu kwa wananchi ambao wengi wao huuza ardhi zao kwa shida.

Walisema utaratibu huo pia unaleta shida kwa wawekezaji ambao hununua ardhi hiyo kwa matumizi mbal mbali.

"Tunajua kwamba serikali ina taratibu zake katika kufanya mambo yake, lakini ni vizuri ukaletwa mwongozo ili kabla ya kuanza taratibu za kufuatilia zoezi hilo, iwe tayari wameshatambua ananunua ardhi hiyo na kujua matumizi yake badala ya kupata maelekezo wakati tayari ameshanunua," alisema Wakili wa Kampuni ya Une Kilimanjaro Attorneys, Fatma Ngomuo.

Alisema suala hilo ni lazima lifanyiwe kazi kwani kufanya hivyo kunaleta shida kwa wao wanaosimamia shughuli hiyo pamoja na wananchi kwa jumla.

Sambamba na hayo, mawakili hao waliomba kuangalia uwezekano wa kuwashirikisha masheha katika hatua za awali za uuzaji wa ardhi kwenye maeneo wanayoishi ili kuepusha migogoro.

Wakili Masoud Hamidu Rukazibwa, alisema pamoja na kuweka katazo la masheha hao wasijihusishe na suala hilo, lakini kutokana na kuwa wao ndiyo wanaojua mipaka na maeneo ya wananchi wao ni vizuri wakashirikishwa.

"Bado masheha wana haja ya kuhusishwa katika hilo kwani kuna wakati tunataka ushuhuda juu ya umiliki kabla ya kufanya uhaulishaji lakini anashindwa kukujazia kwa madai wao wanachotakiwa kujaza ni katika fomu ya uhaulishaji pekee", alisema wakili huyo.


MIAKA MIWILI YA UONGOZI WA MAMA
WAFANYABIASHARA
MANYANYASO
ASANTE RAIS WETU DKT. SAMIA SULUHU HASSANI SIKU HIZI TUNAFANYA BIASHARA ZETU RAHA MSTAREHE
Katuniz KIUELEKEO
@Muhidini Msamba
+255656122770
TOKA RAIS WETU MPENDWA ANDELEE KUKUSOMESHEA WANAO BURE SHULE YA MSINGI, SEKONDARI NA VYUO VYA UFUNDI NDIO UKESHE KWENYE POMBE SIO TABIA NZURI
KITAA
NILIKUWA NAMWAGILIA MOYO MZIKI KWA MBALI KIDOGO ILI KUSHEHEREKEA MAMA YETU ANAVYOTUJARI
NDIYO ULEWE HADI UMWAGE KOJO ADHARANI KWELI
YAANI UNAJIONA MJANJA KUNIDANGANYA ETI NIKIKUKUBALI UTAMSOMESHA MWANANGU CHUO CHA UFUNDI KWA PESA YAKO WAKATI RAIS WETU KASEMA ATAWASOMESHA BURE WATOTO 22,000
DU! UKISIKIA KUUMBUKA NDIYO HUKU
NAMPONGEZA SANA AMIRI JESHI WETU MKUU, RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN KWA KUZUIA MANYANYASO TULIO KUWA TUKIFANYIWA WAFANYABIASHARA NA WATU MAPATO
KWELI KABISA SASA TUNAFANYA BIASHARA ZETU BILA WASIWASI
KABLA YA ZUIO LA MAMA, TULIPATA TAABU SANA HADI TUKAKONDEANA KWA MAWAZO KWA KUSUMBULIWA MARA KWA MARA
WENYEWE WALINENEPEANA KAMA MIPIPA HADI WAKAWA WANASHINDWA KUTEMBEA
KUNA MMOJA ALIKUWA ANAKUJA KATIKA BIASHARA ZANGU, TUMBO LAKE LILIKUWA LINATANGULIA KUINGIA MLANGONI NDIYO KIWILIWILI CHAKE KINAFUATA KWASABABU YA UNENE
HAHAHA... WABONGO BWANA
LAKINI JAMANI JAPO MAMA ANATUTETEA NA SISI TUSIMWANGUSHE INATAKIWA TULIPE KODI KWA WAKATI ILI NCHI YETU IENDELEE ZAIDI
KWELI NDUGU YANGU HILO NALO NENO INATAKIWA TULIPE KODI

# Odinga alaani uvamizi wa shamba la Uhuru Kenyatta

**NAIROBI, Kenya.**

KIONGOZI wa Muungano wa Upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, amelaani uvamizi wa mali ya aliyekuwa Rais wa taifa hilo, Uhuru Kenyatta.

Katika mahojiano na mwandishi wa BBC Ferdinand Omondi, kiongozi huyo wa upinzani alisema anaamini shambulio hilo lilitekelezwa na 'majangili' waliokodishwa na serikali.

Jumatatu ilikuwa siku ya pili ya maandamano dhidi ya serikali yaliyoitishwa na Odinga kwa madai kwamba kulikuwa na udanganyifu katika uchaguzi uliopita pamoja na kupanda kwa gharama ya maisha nchini humo.

Kenyatta ni mshirika wa karibu wa Odinga hivyo kuporwa kwa shamba lake, kunaonekana kama kulipiza kisasi hatua yake ya kumuunga mkono Odinga.

Maandamano zaidi yanapangwa, siku ya Alhamisi wiki hii. Lakini serikali imelaani ghasia na usumbufu unaosababishwa na maandamano hayo.

Odinga aliambia BBC kuwa hajahusika na uharibifu wa mali na waandamanaji na alitetea haki ya Kikatiba ya kuandamana.

Anasema ni bahati mbaya kwamba waandishi wa habari walilengwa na polisi na waandamanaji wakati wa maandamano ya Jumatatu.

Alikosoa baadhi ya sera za kiuchumi za Rais William Ruto, akisema ingawa gharama ya maisha ni tatizo la ulimwengu wote, nchi nyingi zimejaribu kuwaokoa raia wao kutokana na mdororo wa kiuchumi, lakini utawala wa Ruto umeondoa ruzuku na wananchi wanateseka zaidi sasa.

> **Odinga aliambia BBC kuwa hajahusika na uharibifu wa mali na waandamanaji na alitetea haki ya Kikatiba ya kuandamana.**

Odinga alisema yuko tayari kukutana na Rais Ruto kwa mazungumzo, lakini akataja masharti mawili yanayohitaji kuafikiwa. Kwanza, sera za uchaguzi za kielektroniki zifunguliwe ili kuthibitisha ikiwa kura ya mwaka jana iliibiwa na pili kwamba uteuzi wa makamishna wapya wa Tume ya Uchaguzi unapaswa kuhusisha pande zote.



**Raila Odinga**

Mahakama Upeo ya Kenya, ilitupilia mbali kesi ya Odinga kupinga kushindwa kwake katika uchaguzi wa Agosti, mwaka jana, lakini bado anasisitiza kuwa uamuzi huo uliathiriwa.

**BBC**

# ...Tume ya AU yaomba utulivu Kenya

MWENYEKITI wa Tume ya Umoja wa Afrika (AU), Moussa faki Mahamat, ameonesha wasiwasi wake kuhusu ghasia zilizotokea na kusababisha kifo cha mtu mmoja huku mali ya thamani isiojulikana ikiharibiwa kufuatia maandamano dhidi ya serikali.

Katika taarifa iliotiwa saini na Umoja huo, Mwenyekiti huyo sasa anataka wadau kuweka utulivu na kuanzisha mazungumzo ili kuangazia tofauti zilizopo kwa lengo la kuleta umoja na maridhiano.

Aidha, amewakumbusha Wakenya kuhusu ufanisi wa uchaguzi wa Agosti, mwaka jana nchini humo na uthibitisho uliofuatia wa matokeo ya uchaguzi na mahakama ya juu zaidi.

Aliongeza kwamba AU inaunga mkono juhudi za Serikali ya Kenya na raia wake zinazonuia kuleta umoja, amani na uthabiti nchini humo.



**Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), Moussa faki Mahamat**

# Wapiganaji wa Boko Haram waandaliwa maisha mapya

**ABUJA, Nigeria**

MAAFISA nchini Nigeria, wamesema kwamba mpango wa kuwarejesha katika maisha ya kawaida, wapiganaji wa zamani wa kundi la Boko Haram, unasaidia katika kupunguza nguvu ya kikundi hicho.

Karibu wapiganaji 600 wamehitimu mafunzo kuhusu maisha ya kawaida mwishoni mwa wiki na kuomba msamaha kwa umma kutokana na vitendo vyao.

Maafisa wanasema kwamba watasaidiwa kuishi maisha ya kawaida katika jamii, lakini wataalam wanaonya kwamba kuna uwezekano wa watu hao kurudi kwenye mapigano.

Wapiganaji wa zamani 590 wa kundi la Boko Haram walikula kiapo cha utiifu kwa Nigeria, wakati wa sherehe ya mahafali ya kuwaondoa katika maisha ya upiganaji na kuingia katika maisha ya kawaida.

Sherehe ilifanyika Jumamosi iliyopita katika kambi iliyoko Jimbo la Kaskazini la Gombe.

Kundi hilo ni la mwisho la wapiganaji ambao kwa hiari yao, wamekubali kupatiwa mafunzo ya miezi sita ya kiakili na kimwili namna ya kuishi maisha ya kawaida katika jamii.

Maafisa wa Nigeria walianzisha mpango huo Julai, 2016, kama mbinu ya kulimaliza nguvu kundi la wapiganaji la Boko Haram.

"Mafunzo hayo ya kiakili, yamewasaidia watu hao kuwa watu wazuri katika jamii na wamebadilika ikilinganishwa na muda walipowasili katika kambi. Baada ya mafunzo, wanasaidiwa kuishi maisha ya kawaida katika jamii zao," alisema Nnabuihe.

Maafisa wamesema kwamba watu watatu kati ya wale waliomaliza mafunzo hayo, wanatokea nchini Niger na Chad.

Wengine ni raia wa Nigeria kutoka Majimbo ya Borno, Adamawa, Yobe, Zamfara, Niger na Nassarawa.

Wapiganaji hao wa zamani wameomba msamaha kwa umma na kuahidi kusimamia amani katika jamii zao.

Mtaalam wa usalama, Senator Iroegbu, anasema mpango huo unaweza kusaidia kinadharia, lakini huenda kukatokea visa vya watu hao kurudi katika mapigano

"Kutubu ni kitu cha kifikra. Mtu anaweza kujifanya kwamba ametubu kwa sababu ya mazingira yanayomzunguka na kujieleza mwenyewe. Huu ni mpango wenye utata kwa namna nyingi. Kutakuwepo hali ya kusita sita katika kukumbatia mpango huo.

Lakini mwaka 2021, Gavana wa Jimbo la Borno, Babagana Zulum, alitoa mwito wa kutaka mpango huo kufanyiwa tathmini, akisema kwamba waliokuwa wapiganaji wa Boko Haram, wanakusanya taarifa kutoka kwa watu wa kawaida na baadaye kujiunga tena na kundi hilo.

Watu wa kawaida katika Jimbo la Borno ambako ndiyo kitovu cha mashambulizi ya kundi la Boko Haram, wameutilia shaka mpango huo, kama anavyoeleza Vivian Bellonvu, kutoka shirika la Social Action Nigeria.

**BBC**

# Pata nakala laini ya gazeti lako la Uelekeo

## Kila siku ya Jumatano uhabarike

**Habari | Makala | Michezo na Burudani**



Uelekeo Spoti
Leo yetu ndiyo kesho yetu
Irene Paul ataka wasanii Bongo Muvi wasilaumiwe

Uelekeo
Leo yetu ndiyo kesho yetu
UCHUMI
Taifa Stars yapania kuiduwaza Uganda Misri

Maridhiano ya kisiasa TZ
KWA MANDELA 'WAVALIA VIBWAYA'
Dk. Samia aahidi kuyasimamia

Wahitimu wahadharishwa ushoga

Ziara ya Chongolo Singida yawaibua wakulima alizeti

Tanzania yauza nje mazao ya Sh. trilioni 6.

Mradi wa mafuta wamwaga ajira

# Hongera Mheshimiwa Rais

## Miaka 2

## ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania

## Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

Tunakutakia kila la kheri katika kazi zako za kuongoza taifa la Tanzania kuelekea kufikia mafanikio zaidi.



Na Mwandishi Wetu

PICHA za Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Imani Kajura alizopiga akiwa na bosi mwenzake wa Mamelodi Sundowns zinaweza kuwekewa maelezo kadri ya upeo wa mtazamaji.

Zimefanana na zile zote zilizopigwa msimu ule kule Misri. Barbara Gonzalez akiwa Mkurugenzi wa Simba akiongozana na Mjumbe mmoja wa Bodi, wakiikagua miundombinu ya Klabu kongwe ya Al Ahly.

Miaka 15 iliyopita na kurudi nyuma, zisingeweza kupigwa picha za aina hii. Timu zetu zilikua ni kama visiwa vilivyozungukwa na maji mengi.

Zilikua ni timu zilizodaiwa kufanya aina ya mageuzi kwanza ili ziweze kuwa na mipango inayolenga mbali. Mtendaji Mkuu anapofunga safari kwenda Afrika Kusini, nyuma yake zipo baraka za mageuzi ya usimamiaji wa timu.

Anakwenda kule kujifunza namna mpira wa kisasa unavyosimamiwa kwa umakini na kuja na matokeo yenye mtiririko wa kudumu.

Alikwenda kujifunza aina ya uchawi wa kisayansi unaoinua mpira wa mataifa mengine na kuwa na matokeo ya kudumu na kiwango kisichoshuka kwa ubora mwaka baada ya mwaka, bila kujali matokeo ya mechi uwanjani.

Hivi majuzi Klabu ya Simba, imetangaza mpango kazi wa kukuza soka la vijana. Inategemewa kutumika sh. milioni 500 kama bajeti ya mchakato huu mzima. Hakijawahi kusikika kitu kama hiki kutoka kwa viongozi wa klabu zetu hizi mbili.

Ni mpango unaohusisha nchi nzima. Kwamba Simba inashuka huko chini na kutafuta wachezaji wenye umri mdogo kwa ajili ya Hawa kina Jonas Mkude, Abdallah Seseme, Mohamed Hussein, Said Ndemla na wengine waliolelewa na Klabu ya Simba ni matunda ya uongozi wa kabla ya mageuzi Walilelewa katika mfumo wa timu iliyojiendesha kwa njia zisizo rasmi za utafutaji wa vyanzo vya mapato. Heshima maalum na iwafikie watu wa mpira halisi, waliojitolea kuwatafuta vijana hawa na kuwaweka pamoja.

Makofi maalum na yamfikie Kocha Suleiman Matola na wengine waliokuwa walezi wa vijana hawa.

Kuna watu wengi wa aina hii wenye mapenzi ya kweli ya mchezo, ingawa wamekua wakikwazwa na huu urasimu unaoletwa na wavamizi wa mchezo walioibuka na kujaa katika miaka ya karibuni.

Liliandaliwa kundi kubwa la wachezaji, lakini wengi wao wakiwa ni vijana wa hapa hapa Dar es Salaam. Waliweza kupatikana kwa urahisi, wakitokea nyumbani na kwenda kufanya mazoezi ya pamoja.

Huu mpango kazi mpya unakuwa na baraka ya pande zote mbili, zenye kuiongoza Klabu ya Simba kupitia Wajumbe wa Bodi.




**Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu ya Simba, Salum Abdallah 'Try Again' (kushoto) akionesha jezi itakayotumiwa na timu ya vijana ya klabu hiyo, baada ya kuingia mkataba wa miaka mitano kwa sh. milioni 500 wenye kaulimbiu ya 'The Future Is Now'. Picha na Mtandao**

# Mpira wa vijana umekuwa Siasa kwa muda mrefu sasa ni uhakika

> **Liliandaliwa kundi kubwa la wachezaji, lakini wengi wao wakiwa ni vijana wa hapa hapa Dar es Salaam. Waliweza kupatikana kwa urahisi, wakitokea nyumbani na kwenda kufanya mazoezi ya pamoja...**

Ni suala lenye upana na ukubwa kulinganisha na jinsi walivyopatikana hawa wachezaji waliofikia umri wa kuwa waandamizi ndani ya misimu ya karibuni. Simba wanakwenda kuifanya kazi ya kukuza kiwango cha soka cha Tanzania.

Inakuja kuwa ni sehemu halisi ya chanzo cha vipaji hivyo, kurahisisha sana kazi ya makocha wa timu za vijana za taifa na wale wa klabu yenyewe.

Nakumbuka namna Kocha Mbrazil Marcio Maximo, alivyokutana na ugumu wa kufundisha alipogundua kwamba hatukuwa na mfumo wa kueleweka wa uvumbuaji wa vipaji.

Alipozitazama Klabu za Simba na Yanga, hakuona timu zenye msingi mzuri wa wachezaji waliopata mafunzo ya soka tangu utotoni.

Akaanza kufanya kazi kwa uzoefu wake mwenyewe akamuita, Jerry Tegete katika kambi ya Taifa Stars akiwa bado ana akili na mwili wa mwanafunzi wa kidato cha sita.

Miaka mitatu au minne ijayo Kocha wa Stars, atakutana na wingi wa wachezaji wenye miaka 20 ya mwanzo waliopita njia sahihi za malezi ya vijana.

Hatakua na kisingizio cha kueleweka iwapo timu yake itashindwa kupata matokeo katika mechi za kimataifa.

Simba imeamua kutimiza wajibu wake wa kimpira. Ni aibu kwa taifa letu, kuwa linategemea baadhi ya wachezaji wanaoandaliwa na TFF wenyewe pale Uwanja wa Karume.

Yanayofanyika mahali pale ni ya kuzoeleka kufanyika katika viwanja vya mazoezi vya Bunju B na vile vinavyotumiwa na Yanga.

Azam wametumia nguvu kubwa katika kutengeneza wigo wa wachezaji vijana, wanaoandaliwa katika mazingira ya klabu ya soka. Simba kwa ukongwe wao na uzoefu wa masuala ya kimpira, itakwenda kuongeza wigo wa wachezaji wa uhakika.

Natumaini Mkurugenzi wa Simba, Imani Kajura anavyopiga picha na Wakurugenzi wenzake wa klabu kubwa Afrika anapata wasaa wa kutengeneza njaa ya kutaka kuona yanayofanyika huko na hapa kwetu yawe yanafanyika pia.

Mamelodi Sundowns wanamuingiza uwanjani mchezaji mwenye miaka 16, ili acheze mechi ya ushindani ya Ligi Kuu Afrika Kusini, hili pia linawezekana hata hapa kwetu.

Ni kuingia kisayansi kwa asilimia 100 katika kufanya michakato ya maandalizi ya timu za vijana.

# Messi awindwa na klabu 29 Ligi Kuu Marekani

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI nyota wa Paris Saint Germain (PSG) na Argentine Lionel Messi, anawindwa na klabu 29 zinazocheza Ligi Kuu Marekani.

Klabu zinazotaka huduma ya Messi zina imani baada ya mkataba wake na Paris Saint-Germain kumalizika zitamnasa.

Hata hivyo, zipo taarifa Messi (35) anajiandaa kurejea Barcelona katika usajili wa majira ya kiangazi mwishoni mwa msimu huu.

Chanzo kutoka Hispania, kimesema klabu za Marekani zimejipanga kuungana kumvuta nchini humo na yeye ataamua anataka kuitumikia ipi.

Inter Miami inapewa nafasi kubwa ya kumsajili Messi, baada ya mkataba wake kumalizika Juni mwaka huu.

Lakini, klabu inayomtaka italazimika kuvunja benki kumlipa Messi mshahara wa dola za Marekani milioni moja kwa wiki.

Klabu zingine Marekani zinazowania saini ya Messi ni Miami, New York, Los Angeles na Atlanta, ambayo ina mchezaji mwingine raia wa Argentina Thiago Almada.

David Beckham ni mmiliki mwenza wa Inter Miami inayonolewa na nyota wa zamani wa Manchester United Phil Neville, angependa kumuona Messi akijiunga na klabu hiyo.






# Borussia Dortmund yamwania kinda wa Ireland

**LONDON, England**

KLABU ya Borussia Dortmund, wanataka kumsajili kiungo wa kati wa Ireland Kaskazini mwenye umri wa miaka 19 Shea Charles kutoka Manchester City.

Nayo Klabu ya Barcelona italazimika kusajili angalau wachezaji watatu hadi wanne kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto na kufanya kazi ndani ya bajeti ndogo ya mishahara.

Katika hatua nyingine Klabu ya Manchester City, haina mpango wa kumuuza kiungo wake wa kati wa Uingereza Kalvin Phillips msimu huu wa joto, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kucheza mechi chache tangu kuhamia Ettihad kutoka Leeds United.

Hata hivyo, Phillips anasemekana kuwa atakua tayari kuondoka City huku kukiwa na hofu kwamba kukosa muda mwingi wa kucheza, kunaweza kuathiri nafasi yake ya kuchaguliwa kwenye kikosi cha England.




# Saka kuikamua Arsenal pauni milioni 15

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI Bukayo Saka, anaweza kuikamua Arsenal pauni milioni 15 msimu huu endapo atatia saini mkataba mpya na washika bunduki hao wa jiji la London.

Saka (21) amekuwa shujaa wa Klabu ya Arsenal na timu ya taifa ya England, baada ya kucheza kwa kiwango bora msimu huu.

Juzi usiku, alithibitisha ubora wake baada ya kuchangia ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ukraine, katika mechi za kufuzu Fainali za Ulaya. Saka anatarajiwa kupata mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki, endapo atatia saini mkataba mpya Arsenal.

Endapo nyota huyo atamwaga wino, atakuwa ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa katika Klabu ya Arsenal inayoongoza Ligi Kuu England. Kiungo wa zamani wa klabu hiyo Mesut Ozil, aliwahi kulipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki Arsenal.

# Conte kupeleka makali yake Ligi Kuu ya Italia

**LONDON, England**

KOCHA Antonio Conte anatarajiwa kupeleka makali katika Ligi Kuu ya Italia 'Serie A', baada ya kutupiwa virago kwenye Klabu ya Tottenham Hotspurs.

Sare ya mabao 3-3 iliyopata Spurs dhidi ya Southampton, ilihitimisha kibarua cha kocha huyo baada ya kudumu Makao Makuu White Hart Lane kwa miezi 16.

Kauli anayodaiwa kuitoa, Conte ya kuwaita wachezaji wake wabinafsi, huku akiwataja mabosi wake kwamba hawana utamaduni mzuri, ulimuweka matatani kabla ya juzi kumalizana. Wakati Conte akifungasha virago, Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy anamtaka Kocha Julian Nagelsmann kujaza nafasi ya Mtaliano huyo mwenye miaka 53.





Wachezaji wa timu za Skuli ya Msingi wa Turkey na Wazazi, wakigombaniana mpira katika mchezo wa fainali ya Elimu bila Malipo ngazi ya wilaya, uliochezwa Uwanja wa Zimamoto, Wazazi walishinda kwa pointi 40-5. Na Mpigapicha Wetu

# Vijana Zanzibar washauriwa kujifunza gofu

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

VIJANA nchini wameshauriwa kujitokeza kwa wingi katika kujifunza mchezo gofu, ili Zanzibar irudi kwenye hadhi yake kama ilivyokua hapo awali.

Ushauri huo ulitolewa na mchezaji mahiri wa gofu visiwani hapa, Mussa Foum Haji wakati alipozungumza na mwandishi wa habari hizi kuhusiana na mchezo huo, ambao unaonekana kupotea.

Alisema kwa miaka mingi, vijana wamejikita katika kucheza soka na michezo mengine na kuachana na gofu ambao ni mmoja wa michezo maarufu na iliyoitangaza vyema nchi.

"Ushauri wangu kwa vijana kujitokeza kwa wingi kujiunga na mchezo wa gofu ambao hivi sasa, umekosa hadhi kama iliyokuwepo hapo awali," alisema.

Mussa ambaye kwa sasa ni mchezaji pekee wa gofu visiwani hapa alisema, endapo vijana watajitokeza kucheza gofu wataweza kupata mafanikio yao binafsi na hata nchi kwa ujumla.

## Azungumzia changamoto Mashindano Elimu bila Malipo

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

MRATIBU wa Michezo Wilaya ya Mjini, Mohammed Ali Abdalla amesema licha ya changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa Mashindano ya Elimu bila Malipo, lakini wanashukuru yamekwenda vizuri na kuonesha ushindani kwa timu zote shiriki.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mashindano hayo wilayani Mjini Mratibu huyo alisema kwa ujumla yalikua na ushindani wa hali ya juu na vijana walionesha vipaji vilivyovutia wengi.

"Katika mashindano, hayo ambayo yalichezwa kwa mtindo wa mtoano yalikuwa na changamoto za hapa na pale lakini yamekwenda vizuri na ushindani ulikua mkubwa," alisema Mratibu huyo.

Alisema kutokana na ushindani ulioonesha kila timu ilitolewa wakati wa kutafuta 'best Looser' ilikuwa iking'ang'ania kuwa ipewe nafasi ya kucheza lakini kwa kuwa kuna vigezo maalumu, ilibidi apewe ambaye alifikia vigezo hivyo.

## Sekondari Lugoba yaita wadau kusaidia vifaa vya michezo

**Na Mwandishi Wetu, Chalinze**

UONGOZI wa Shule ya Sekondari Lugoba iliyopo Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, imesema inakaribisha wadau wa kucheza kujitokeza kusaidua vifaa mbalimbali vya michezo.

Ombi hilo lilitolewa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Abdallah Sakasa wakati akizungumza na waandishi wa habari shuleni hapo, ambapo alisema shule iko mstari wa mbele katika michezo lakini inakabiliana na upungufu wa vifaa.

Alisema shule ina viwanja vya kutosha vinavyotumika kwa ajili ya michezo mbalimbali, huku akieleza kuwa kati ya hivyo ni kimoja pekee cha mchezo wa basketi ndiyo chenye changamoto na kwamba wanaangalia namna ya kuuboresha.

"Katika Halmashauri yetu ya Chalinze shule yetu ya Lugoba imechaguliwa kuwa kitalu cha mchezo wa netiboli, wachezaji wote wa mchezo huo wanafika hapa kwa ajili ya mazoezi tayari kwa mashindano," alisema.



# Beyonce, Adidas wakubaliana kuvunja mkataba


**NEW YORK, Marekani**

NYOTA wa muziki nchini Marekani, Beyonce na Kampuni ya Adidas wameripotiwa kukubaliana kuacha ushirikiano wao ambao ulikua baina ya Adidas na Kampuni ya Beyonce ya mavazi ya Ivy Park.

Kwa mujibu wa chanzo kilicho karibu na mazungumzo ya biashara kilisema, nyota huyo mwenye umri wa miaka 41 na kampuni hiyo ambayo hutengeneza nguo za michezo ambayo inatoka nchini Ujerumani, walifanya uamuzi wa pande zote mbili wa kusitisha ushirikiano huo kwa mujibu wa The Hollywood Reporter.

Mwanamuziki huyo na Adidas, walianza ushirikiano wao mwaka 2018 wakati ambapo Adidas walichukua jukumu la kutengeneza nguo za Ivy Park, wakati Beyonce pia alifanya kazi ya viatu na nguo kwa chapa hiyo maarufu duniani. Habari za kuvunjika kwa ushirikiano huo wa kibiashara, zinakuja baada ya jarida la Wall Street Journal kuripoti Februari mwaka huu, kwamba Kapuni ya Mavazi ya Beyonce ya Ivy Park, ilifanya biashara na kuingiza takriban dola za Marekani milioni 40 pekee, ikilinganishwa na matarajio ya awali ya mauzo ambayo yalitarajiwa kuwa ni dola milioni 250 kulingana na chanzo cha THR.

Imeelezwa pia Beyonce na Adidas, walitofautiana kuhusu tofauti za ubunifu hivi karibuni na kusababisha



## Beyonce, Adidas wakubaliana kuvunja mkataba

Uk. 23

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumanne Machi 22 - 28, 2013 |




## Saka kuikamua Arsenal pauni milioni 15

Uk. 21

# Kocha Julio amtaka MO Dewji kuwabadilisha watendaji Simba

## Mwenyewe asema 'atawashitaki' kwa wanachama

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEWAHI kuwa mchezaji wa Simba na pia Kocha wa klabu hiyo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amemtaka Rais wa Heshima wa Simba Mohamed Dewji 'MO', kuwataja wanaomkwamisha katika uwekezaji wake kama mwenyewe anavyosema.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Julio alisema MO ndiye mwekezaji na yeye ndiye aliowaweka madadakani anaodai wanamkwamisha, hivyo cha msingi ni kuwaondoa na kuwabadilisha ili kuwaleta watu wengine wanaoitakia mema Simba.


Julio


Dewji

Alisema MO hao anawajua watu hao na si sawa kuendelea kuwakumbatia madarakani, kama anaona wanakwamisha mchakato wa mabadiliko awataje majina kwa kuwa yeye ana nia nzuri, isipokua kuna wanaokwamisha halafu lawama anatupiwa yeye.

"Watu hao wanatakiwa waondoke kama ilivyo kwa aliyekua Rais wa kwanza, Hayati Julius Nyerere ambaye alimpisha Ali Hassan Mwinyi na yeye alimwachia, Marehemu Benjamin Mkapa, baadaye akaja Jakaya Kikwete na hatimaye, Marehemu John Magufuli na sasa Mama Samia Suluhu Hassan anaendelea," alisema. Alisema MO kwa fedha alizonazo au kwa Klabu za Yanga na Azam, hazishindwi kwenda kuchukua mchezaji yeyote duniani kutokana na uwezo wa kifedha wanaokeza katika timu hizo kwa kuwa hizo zina wawekezaji ambao wanatakiwa kuwa na uwekezaji wa maana.

Hatua hiyo ya Julio imekuja baada MO, kutamka wazi katika mitandao ya kijamii kwamba kuna watu ndani ya Simba wanakwamisha mchakato wa mabadiliko, ila ana imani endapo mchakato utakamilika watafikia malengo waliojiwekea.

MO alisema wanajipanga kuijenga Simba upya kwa ajili ya miaka mitano ijayo kwa kuwa nia yao ya usajili kwa wakati huu imefeli.

Alisema uzuri ni kwamba watu hao anawajua na kama wataendelea kukwamisha mchakato huo atatoka hadharani kuwataja kwa majina ili kuachia hatima yake na hao wanaokwamisha suala hilo kwa wanachama.

Akizungumzia usajili, MO alisema kuna makosa yamefanyika hasa katika suala hilo lakini pia anaangalia uwezekano wa kutafuta 'maskauti' bora kutoka nje ya nchi, ambao watashirikiana na maskauti wa ndani ili kubadilisha mfumo kwani anaamini wataifanya kazi yao kwa ubora zaidi tofauti na kama inavyofanyika sasa.

"Tunaamini endapo tutabadilisha mfumo wa usajili kwa kuwaleta 'maskauti' wazuri tuna uwezo wa kupata wachezaji wazuri watakaoifikisha timu katika malengo tuliojiwekea," alisema.

Hata hivyo MO aliwahi kunukuliwa na vyombo vya habari akidai kwamba pesa zake zinapotea kwani hapati faida, mpaka sasa ametumia zaidi ya dola za Marekani milioni 20 bila kupata faida, kwani amewekeza kutokana na mapenzi aliyonayo kwa Simba lakini klabu hiyo haimuingizii faida yoyote huku watu wakimtupia lawama kwamba hajaingiza chochote.

Wakati huo huo, Meneja wa Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally alisema kikosi cha timu hiyo kiliondoka jana saa 9 alasiri kikiwa na wachezaji 15 kwenda Morocco kuikabili Klabu ya Raja Casablanka katika mechi ya Kundi C ya Klabu Bingwa Afrika hatua za makundi itakayochezwa Uwanja wa Mfame wa Tano Jumapili nchini humo.

Alisema lakini wengine 13 waliopo katika timu zao za taifa watajiunga moja kwa moja na kikosi hicho kujiunga na kikosi hicho wakitokea katika nchi zao.



## Nabi: Kujiamini kwa wachezaji inatupa jeuri kuongoza kundi

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Yanga, Nasreddin Nabi amesema kinachoipa nguvu timu yake na kuongoza Kundi D katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika mbele ya Waarabu wa Tunisia, US Monastri ni kujiamini kwa wachezaji pamoja na ushirikiano.

Yanga kwenye michuano hiyo inaongoza kundi hilo na mchezo wake uliopita iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya US Monastri mchezo wa Jumapili watakaibili TP Mazembe Lubumbashi, DR Congo.

Timu hizo katika mchezo uliochezwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam ubao ulisoma Yanga 3-1 TP Mazembe, hivyo mchezo huo wa Jumapili kila timu itakua na kazi ya kusaka pointi.

# ZFF kuendelea kudai uanachama wake CAF

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), limesema litaendelea na harakati zake za kudai uanachama wake kwenye Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kwa kuamini wao bado ni wanachama halali kwa kuwa vigezo vilivyotumika kutolewa havikufuata utaratibu wa kisheria.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi ofisini kwake Katibu wa ZFF, Hussein Ahamada Vuai alisema historia inaonesha Zanzibar iliwahi kuwa mwanachama wa CAF na kuondolewa bila ya kufuatwa utaratibu wa kisheria kwa mujibu wa katiba ya CAF.

Alisema Zanzibar, ilipata uanachama huo mwaka 2017 kwa kufuata utaratibu wa namna ambavyo mwanachama anapaswa kuwa mwanachama kwa kufanyika Mkutano Mkuu na kupigiwa kura na kupata kura 51 kati ya nchi 54 .

"Utrataibu wote wa kisheria wa kuingia ulifuatwa kwa mujibu wa katiba, lakini walivyotolewa hakuna Mkutano Mkuu wala hakuna kumbukumbu yoyote, hivyo hakukufuatwa taratibu," alisema.

Alisema mantiki hiyo, anachokiamini Zanzibar bado ni mwanachama na wanafanya jitihada zao kuona wanarejeshewa uanachama katika uhalisia wake.

Katibu huyo aliseema, katika jitihada zao hatua zipo vizuri na wameshafanya mazungumzo ya moja kwa moja na Katibu Mkuu CAF katika vikao mbalimbali ambavyo Zanzibar wamekua wakishiriki kupitia CAF na Baraza la Michezo kwa Nchi za Afrika Mashariki na Kati (CEFACA).

"Kwa hiyo tumepata ushirikiano mkubwa mpaka sasa, zilizobaki ni hatua za kisheria na kikanuni kuona tunarejeshwa vipi, ila kwa hatua tumeshaanza mazungumzo na kuwaandikia CAF moja kwa moja na tunasubiri maelekezo," alisema.

Zanzibar ilipata uanachama wa CAF mwaka 2017 na kuondolewa ndani ya kipindi kifupi hali iliyoleta sintafahamu kwa wananchi na wadau wa michezo visiwani hapa.